# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 7, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581730

JUMAPILI

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13

**UNATAKA KUMPAGAWISHA?**

**Aliyekuwa** Ofisa Usalama wa Taifa ashtakiwa kutuma watu kuua mkewe

UKURASA 2




**Muhimbili** yabuni ajira kwa waraibu dawa za kulevya

UKURASA 4

MAISHA YALIVYO

**Ujue** undani wa maisha ‘wabongo’ wanaokwenda kusoma ughaibuni

UKURASA 11



Katibu wa NEC ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla.



Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe.

# CCM: Mbowe ajiandae kujiuzulu CHADEMA

• **Yatamba** kuwatumia kina Msigwa kufanikisha... *ukurasa 3*

UKURASA WA 17

## WANAJESHI 27 DRC WAHUKUMIWA KIFO

## Watoto wadaiwa kujiteka, kushinikiza wazazi wao kutuma fedha waachiliwe

UKURASA 5



Mwendesha pikipiki maarufu Bodaboda, akiwa amepakia abiria wanne, mjini Bariadi, mkoani Simiyu jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mchungaji mbaroni tuhuma za mauaji na kupora gari

UK. 2

**MICHEZO** **MASHINE ZA YANGA ZATUA NCHINI** UK.24

**MAONI,** UK.6

## Aliyekuwa Ofisa Usalama wa Taifa ashtakiwa kutuma watu kuua mkewe

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri umedai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa aliyekuwa Ofisa Usalama wa Taifa (jina tunahifadhi kwa sababu za kisheria), alituma vijana wawili kumvamia mke wake, Atusege Kitalamo nyumbani kwake na kumchinja hadi kufa kutokana na imani za kishirikina.

Mbali na mshtakiwa huyo, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Roger Shaban, maarufu Mayala (25), na Furaha Ng'amba (47), wote wakazi wa Wilaya ya Urambo, mkoani Tabora.

Wakili wa Serikali Neema Musho alidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Franco Kiswaga aliyepewa mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Na wakati akiwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika.

Wakili Neema alidai kuwa washtakiwa wote watatu wanashtakiwa kwa kosa moja la mauaji ya Atusege.

Inadaiwa kuwa Disemba 12, 2020, wakati wa usiku, washtakiwa Shabani na Ng'amba walivamia nyumba hiyo, wakamchukua na kumpeleka kwenye mto wa karibu na kumchinja hadi kufa baada ya kuelekezwa na mumewe (50), mauaji hayo yakihusishwa na imani za kishirikina.

Ilidaiwa kuwa siku iliyofuata, mwili wa marehemu ulipatikana kwenye mto huo karibu na nyumba ya marehemu. Taarifa hiyo iliripotiwa katika Kituo cha Polisi Goba, askari polisi walikwenda eneo la tukio na kuchora ramani ya tukio.

Wakili Neema alidai kuwa mwili wa marehemu ulipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala hadi Disemba 15, 2020 uchunguzi wa postmortem ulipofanyika na daktari katika ripoti yake alieleza kuwa chanzo cha kifo cha mama huyo kilitokana na kuvuja damu nyingi na majereha ya kina.

Baada ya hapo, Wakili Neema alidai kuwa washtakiwa walikamatwa na askari polisi wa Urambo, Tabora na baada ya kuhojiwa, katika maelezo yao ya onyo walikiri kutenda kosa hilo, walipelekwa kwa mlinzi wa amani ambako pia walikiri kutenda kosa.

Baada ya upelelezi kukamilika, washtakiwa hao walifikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka yao. Wakili Neema alidai mahakamani huko kuwa watakuwa na mashahidi 24 na vielelezo 11.

Mshtakiwa wa kwanza anatetewa na Wakili Selemani Matauka, Mshtakiwa wa pili anatetewa na Ramadhani Makange na wa tatu anatetewa na Hilda Mushi.

Washtakiwa wamerudishwa rumande kusubiri kupangwa tarehe ya usikilizwaji Mahakama Kuu.

# Mchungaji mbaroni tuhuma za mauaji na kupora gari

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MCHUNGAJI wa Kanisa la T.A.G Kata ya Buhongwa, jijini Mwanza, George Masangya (35) anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya Majuto Mabula (38), Mkazi wa Mtaa wa Usagara, mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Willbroad Mutafungwa alisema jijini hapa juzi kuwa mauaji hayo yalitokea Juni 28 mwaka huu, saa tano asubuhi katika Mtaa wa Lugeye, wilayani Ilemela.

Kamanda Mutafungwa alisema Mabula alifikwa na umauti baada ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili wake kisha mwili wake kutelekezwa katika shamba la mahindi.

Alisema kuwa baada ya mauaji hayo, watuhumiwa walipora gari lenye namba ya usajili T 851 ECU aina ya Toyota Ractis, mali ya Bertha Yohana na kutokomea nalo kusikojulikana.

"Baada ya kupokea taarifa, tulianza upelelezi wa kina na kufanikiwa kumkamata George Masangya akiwa amejificha mkoani Arusha kukwepa mkono wa sheria," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi pia alisema wanashikilia watuhumiwa wengine wanaodaiwa kushiriki kutekeleza mauaji hayo pamoja na wizi wa gari tajwa.

Alitaja watuhumiwa hao ni pamoja na Mwaita Kangara (38), fundi magari na mkazi wa Itebe, Mkoa wa Mara; Machela Mkono (36), mfanyabiashara na mkazi wa Kogete, Mkoa wa Mara; na Marwa Matiko (38), dereva na mkazi wa Msati Highway, Mkoa wa Mara.

Vilevile, Kamanda Mutafungwa alisema jeshi hilo linaendelea kumsaka mtuhumiwa mwingine aliyeshiriki mauaji hayo huku likikamata pia gari lililokuwa limeporwa, likiwa limefichwa mkoani Mara.

"Watuhumiwa wote wanaendelea kuhojiwa kwa kina na watafikishwa mahakamani mara baada ya upelelezi kukamilika," alisema.

Kamanda Mutafungwa pia alisema jeshi hilo linamshikilia Samwel Paul (30), mkulima na mkazi wa Kijiji cha Kaisa, wilayani Sengerema kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya Adam Lukanaza (24), mkazi wa kijiji hicho.

Alisema tukio hilo la mauaji lilitokea Juni 25 mwaka huu, saa moja asubuhi. Lukanaza anadaiwa kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na mdomoni, kisha mtuhumiwa kukimbilia wilayani Bukombe, mkoani Geita kujificha kwa ndugu yake alikokutwa na jeshi hilo.

"Bado tunaendelea kumhoji na pindi upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (CPA), polisi wakishakamata mtuhumiwa, wanapaswa ama wamfikishe mahakamani ndani ya saa 24 tangu walipomkamata au kumwachia huru, isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, makosa yanayowakabili watuhumiwa tajwa hapo juu (kuua kwa kukusudia), yakithibitika, adhabu yake ni kunyongwa hadi kufa.



Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi (wa pili kushoto), akitoa maelezo kwa wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia kuhusu kituo hicho, kinavyojishughulisha na kilimo cha mboga, ili kujiimarisha kiuchumi, walipotembelea kituoni hapo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi, BoT waendesha msako wa taasisi zinazodhalilisha wakopaji

**Christina Mwakangale na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema taasisi za kifedha hasa za mtandaoni ambazo huvujisha taarifa za mkopaji, ikiwamo kutuma ujumbe wa deni la mhusika kwa kila namba aliyohifadhi katika simu, zinakiuka sheria.

Imesema kwa muda mrefu taarifa kuhusu hali hiyo zimeendelea kuripotiwa kutoka kwa wakopaji hao kwamba wanapokopa fedha kutoka taasisi za mtandaoni, hawafahamishwi baadhi ya kanuni za ukopaji huku wakivujishiwa taarifa binafsi kwa rafiki, ndugu na jamaa.

Ofisa Mkuu Mwandamizi Idara ya Usimamizi wa Huduma Ndogo za Fedha BoT, Deogratias Mnyamani, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe Jumapili kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba. Alisema kwamba watoamikopo wote nchini ikiwamo wenye mifumo ya mtandaoni wanaofanya kazi bila usajili na leseni, wanakiuka kanuni za BoT.

Alisema taasisi hiyo imeandaa operesheni ambayo inashirikisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwachukulia hatua wanaokiuka sheria.

"Wengi wanapokopa hawana nakala ya mkopo, wanapojisajili, akiwa na NIDA anakamilisha usajili mtandaoni haraka kwa sababu ana shida na fedha, kuna baadhi ya masharti na vigezo hasomi, pengine lugha si rafiki, yeye anachoangalia kupata fedha," alisema.

Mnyamani alisema kuwa hadi sasa wana kesi 10 zinazoendelea zikihusiana na makosa ya huduma za fedha kwa mtandao na taasisi zinazotoa mikopo bila kufuata sheria.

Alisema kuwa wanapokea wastani wa malalamiko 10 kwa wiki yanayohusisha wahitaji fedha za mikopo kudhalilishwa au kushikiliwa mali zao kinyume cha makubaliano.

"Watakaobainika watashtakiwa kwa kosa la kivujisha taarifa na siri za watu. Kutuma ujumbe kwa mtu ambaye anatajwa ni mdhamini unakuta hafahamu hata kama kamdhamini mtu, siyo sawa," alisema Mnyamani. Wakati wa kuhitimisha hoja ya mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 bungeni mwishoni mwa mwezi uliopita, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema wamepokea malalamiko ya watu kudhalilishwa wanapokopeshwa na taasisi zinazotoa mikopo mtandaoni.

Alisema kuwa serikali inafuatilia nyendo zao; polisi, BoT na TCRA wameungana kushughulika na kundi hilo kwa hatua zaidi za kisheria.

## HABARI KITAIFA

# CCM: Mbowe ajiandae kujiuzulu CHADEMA

**Na Romana Mallya**

KATIBU wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amemtaka Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe kujiandaa kujiuzulu.

Hiyo ni baada ya hivi karibuni Mbowe kujiapiza kuwa ataachia ngazi ikiwa chama chake kitashindwa kuyarejesha majimbo ya Kanda ya Kaskazini katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Makalla ambaye pia ni mlezi wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wanachama wa chama hicho ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara ya siku saba mkoani humo.

Akihutubia katika mkutano huo, Makalla alisema amemsikia Mbowe akisema lazima washinde majimbo yote ya Kanda ya Kaskazini na akishindwa atajiuzulu.

"Sasa na sisi tumwambie tumemrekodi kuwa ajiandae kutoka maana sisi tutachukua majimbo yote ya Kaskazini na Tanzania yote. Sisi siyo wabaguzi, tunapiga kote, siyo yeye anabagua, ninajua anajiandaa na uenyeketi, alidai Makalla.

Mwenezi huyo wa CCM alidai vyama vya upinzani vimekosa mvuto na mwelekeo na ndio maana watu wao wanazidi kuhamia chama kinachoongoza serikali, CCM.

"Hapa kuna diwani wa CHADEMA anataka kuja nimpokee na bado tutapiga bomu lingine mpaka wakimbiane," alitamba Makalla ambaye baada ya hotuba yake, alimpokea diwani huyo kutoka Kawe aliyekuwa msaidizi wa Mbunge Halima Mdee.

**MAKUNDI CCM**

Makalla pia alielekeza wanachama wa chama hicho kujiandaa kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani kwa kuvunja makundi ambayo alisisitiza yamekuwa yakikighārimu chama hicho.

Vilevile, alikemea baadhi ya wana CCM kupanga safu za viongozi kwa kuwa kitendo hicho ni kinyume cha taratibu za chama hicho.

Alisema hawawezi kushinda kama hawako pamoja na kueleza kuwa makundi, hila na fitina vinapunguza kura za CCM.

"Wewe umeshachaguliwa kuwa diwani, umechanguliwa kuwa mwenyekiti wa mtaa, umechaguliwa kuwa mbunge, umechaguliwa kuwa mwenyekiti wa wilaya miaka mitano, bado unasaka maadui zako wapi na wapi!

"Uchaguzi ukishaisha mtu bado ni diwani anatafuta wabaya wake, wewe ni mwenyekiti bado wa ngazi fulani, bado unatafuta wabaya wako waliokupinga miaka mitano, visasi havishi.

"Ukishachaguliwa vunja makundi, fanya kazi na watu wote. Na watu wakikupinga ndio demokrasia. Mbona kuna mtu mmoja alikuwa na kura za maoni za mbunge kina (Abbas) Mtemvu anajua hapa Dar es Salaam mpaka mke wake hakumpigia kura?

"Alipomwuliza (mke wake) akasema 'wewe ninakaa na wewe, ninajua udhaifu wako, bora tumpe fulani, ndio maana familia hatujakupa kura'. Kwahiyo, ni demokrasia. Niwaombe tujiepushe na makundi na visasi viishe, tujenge chama chetu," alielekeza.

Makalla alisema chakula cha wanasiasa ni watu na katika hilo amejionea namna wanachama walivyojitokeza kwa wingi katika mkutano huo na kueleza kuwa hiyo ni dalili ya mwazo mzuri.

"Tuendelee hivihivi kwani ndio kwanza tumeanza, lakini wakati nimeteuliwa katika nafasi ya uenezi, nilisema 'nimerudi nyumbani' na leo nimepewa nafasi ya ulezi wa Mkoa wa Dar es Salaam, sehemu ambayo nimeanzia siasa.

"Mpaka sasa ninarudia kusema 'nimerudi nyumbani', pokeeni salamu za Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Makalla.

Kiongozi huyo wa CCM pia alisema chama hicho hakiwezi kujitenga na matatizo ya wananchi na kuwataka watendaji wa serikali, wakiwamo wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi, kuendelea na utaratibu wa kutenga muda kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Makalla pia alisema Mch. Peter Msigwa na Upendo Peneza waliojiunga na CCM hivi karibuni wakitokea CHADEMA, wataanza kuonekana kupitia mikutano ya hadhara ya chama wakieleza alichokiita "ukweli kwa Watanzania", hasa mambo yaliyofanywa na serikali ya chama chao.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Mtemvu, aliwahakikisha wanachama wa chama hicho "ushindi wa kishindo katika uchaguzi ujao".


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Muhimbili yabuni ajira kwa waraibu dawa za kulevya

**Na Romana Mallya**

HUDUMA inayotolewa na waraibu wa dawa za kulevya ya kubeba kwa kutumia viti mwendo wagonjwa wasioweza kutoka lango kuu la kuingilia Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), imebadili maisha yao.

Ni miezi 12 tangu kuanza kutolewa huduma hiyo mwezi Julai mwaka jana, hospitali hiyo ya ngazi ya juu zaidi kitaifa ikiwatumia waraibu hao wa dawa za kulevya kusaidia wagonjwa wasiojiweza, kuwasogeza karibu na huduma wanazokwenda kupata hospitalini huko.

Hao ni waraibu wa dawa za kulevya wanaoendelea na tiba ya methadone hospitalini huko. Hivi sasa kupitia kubeba wagonjwa, wameimarisha hali zao kiuchumi.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma MNH, Aminiel Aligaesha anasema wameona tija ya kuwapa jukumu hilo waraibu wa dawa za kulevya. Anasema Muhimbili hivi sasa inatibu takribani waraibu 1,000. Kati yao, 60 ndiyo wanatoa huduma ya kubeba wagonjwa wasiojiweza hospitalini huko.

"Huduma hii inasaidia sana waraibu wa dawa za kulevya, inawasaidia kujikwamua kiuchumi kulinganisha na kazi walizokuwa wanazifanya huko mtaani.

"Hivi sasa wanaweza kutunza familia zao. Wamekuwa na nidhamu ya kazi na nidhamu binafsi. Imewasaidia kuendelea kuwa watu wema, kujiamini na kuheshimiwa na watu wengine," anasema.

Ubunifu wa Muhimbili, Aligaesha anautaja umepunguza vijana kurudia hali yao ya utegemezi wa dawa na vilevi vingine kama bangi na pombe.

"Hivi sasa ni wasafi sana kimwonekano wa mavazi yaliyofuliwa, kuoga, kuchana au kusuka au kunyoa nywele. Wanakubalika na jamii na hata wenzao wanawakubali kuwa wamebadilika," anasema.



**WAFUNGA NDOA**

Aligaesha anasema huduma hiyo pia imebadilisha maisha yao, akitolea mfano wawili waliofunga ndoa na wale waliokuwa na familia zao, hivi sasa wanazihudumia vizuri.

"Kwa sasa vijana hawa ni watu wenye kujiheshimu, na kuheshimu wengine na wanatumia lugha nzuri," anasema na kubainisha kuwa wana kundi lingine linalopewa majukumu mengine kama vile ufundi selemala na ujenzi, hasa upakaji rangi.

Ofisa huyo wa Muhimbili anabainisha kuwa kupitia huduma hiyo, wastani wa wananchi 150 hadi 170 huhudumiwa kwa siku na vijana hao hospitalini huko sawa na wananchi 750 hadi 850 kwa wiki.

"Asilimia 70 ya wananchi hao wanapelekwa maeneo mbalimbali ya hospitali hii, asilimia 20 Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) na asilimia 10 Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)," anasema.

Aligaesha anasema kuwa katika hospitali hiyo, vijana hao husaidia wagonjwa kuzifikia huduma zikiwamo za dharura, idara ya radiolojia na zinazotolewa katika jengo la wagonjwa wa nje.

Anafafanua kuwa zaidi ya asilimia 50 ya wananchi wanaohudumiwa na vijana hao, hupelekwa idara ya radiolojia, asilimia 30 jengo la wagonjwa wa nje, asilimia 10 jengo la watoto na asilimia 10 jengo la wazazi.

Ofisa huyo anasema wagonjwa hao ni wale wa kawaida ambao hutoka majumbani. Wagonjwa wanaotokana na ajali, wengi wao hupelekwa hospitalini huko kwa kutumia magari ya wagonjwa.

Kuhusu changamoto ambazo hujitokeza katika utekelezaji wa huduma hizo, Aligaesha anazitaja ni pamoja na mwananchi akipewa huduma hiyo hupenda kushinda na mtoahuduma wa kiti mwendo mpaka atakapomaliza matibabu yake.

**WANAOHUDUMIWA**

Selina Emmanuel, mkazi wa Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam, aliyekutwa na mwandishi katika lango kuu la kuingia Muhimbili akiwa na mgonjwa wake, alipongeza hospitali hiyo kwa ubunifu huo, akiutaja unasaidia wagonjwa na watoahuduma (waraibu) kubadilika.

Shughuli wanayoifanya ni kipimo tosha kuona mabadiliko yao. Kama unavyoona wanaturahisishia sisi tunaokuja na watu ambao hawawezi kutembea, wanatuongoza mpaka katika huduma tunayotaka.

"Muhimbili ni hospitali kubwa, ina vitengo vingi, lakini kupitia vijana hawa wanaturahisishia wanambeba mgonjwa wako wanakupeleka moja kwa moja unakoelekea, binafsi ninapongeza ubunifu huu, unawasaidia pia na wao kufuatiliwa kwa karibu na madaktari wao kujua hali zao za matibabu.

"Ukiwaangalia kimwonekano ni wasafi na wana lugha nzuri, huwezi kujua kama wamepitia changamoto hii ya dawa za kulevya," alipongeza.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Juni 30 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani yaliyofanyika viwanja vya Nyamagana, jijini Mwanza, aliagiza kuandaliwe mpango wa kitaifa wa kuwezesha waraibu wanaoachana na matumizi ya dawa za kulevya nchini, kujikimu kimaisha.

Aliagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Waziri Mkuu, kukaa pamoja na Wizara ya Fedha kuandaa mpango huo ambao utawezesha kundi hilo kupata mitaji itakayowawezesha kushiriki katika shughuli za ujasiriamali ili kukuza kipato chao.

"Wako wengine wanaohitaji kilimo, Wizara ya Kilimo itoe utaratibu; wapo wanaohitaji ufundi, Wizara ya Elimu itoe utaratibu, lengo ni kuhakikisha vijana hawa wakitoka huko wanakuwa na shughuli ya kufanya ili kujikimu.

"Kamishna Jenerali pamoja na timu yako ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, endeleeni kufanya operesheni dhidi ya dawa za kulevya katika mabasi, ndege, bandarini, vituo vya reli, masoko, maeneo yenye watu wengi, kote nchini, ili kuhakikisha kuwa tunaendelea kubaki salama.

"Niwahimize wananchi wote wakiwamo wazazi, walezi, viongozi wa dini na taasisi za afya, tuendelee kupiga vita dawa za kulevya kwa vitendo na kuhakikisha jamii yetu haijihusishi na biashara, haifanyi uzalishaji wala matumizi ya dawa za kulevya, ikiwamo kutokomeza kilimo cha bangi na mirungi," aliagiza.

Majaliwa alisema serikali imefanikiwa kujenga zaidi ya vituo 16 vinavyohudumia waraibu 16,460 kutoka vituo vitatu vilivyokuwapo mwaka 2017.

"Leo hii ni siku muhimu sana katika historia ya taifa letu, kwani tutashuhudia uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024.

"Sera hii mpya inaweka msisitizo katika jukumu la kila mmoja wetu kuanzia ngazi ya kaya hadi taasisi za serikali na asasi za kiraia. Hivyo, ninapenda kuwahimiza sote tujitolee kikamilifu kutekeleza sera hii. Tuwe walinzi wa vijana wetu na tukishirikiane, tunaweza kufanikisha lengo la kuwa na jamii salama na yenye afya njema," Majaliwa alihimiza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa, ikiwamo ununuzi wa mashine kubwa na ya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa haraka wa viashiria vyote vinavyotakiwa kupatiwa sampuli na kuthibitisha kuwapo matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema mashine hiyo iko Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, imepata ithibati ya Umoja wa Mataifa na ina uwezo wa kuchukua zaidi ya sampuli 250 kwa siku.

Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia Juni 2023 hadi Mei 2024, mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vyombo vingine, ilikamata zaidi ya kilo milioni mbili za dawa za kulevya, kiwango alichotaja ni kikubwa zaidi katika kipindi cha miaka 11.

HABARI KITAIFA

# Watoto wadaiwa kujiteka, wakishinikiza wazazi wao kutuma fedha waachiliwe

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATOTO wawili wilayani Ilemela, mkoani Mwanza wanadaiwa kutoroka nyumbani kisha kupiga simu kwa wazazi wao wakidai kuwa wametekwa.

Mmoja wao mwenye umri wa miaka 12, anasoma darasa la saba katika Shule ya Msingi Busenga wilayani Ilemela na mdogo wake mwenye umri wa miaka minane ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Akiba wilayani humo (majina yao tunahifadhi kwa sababu za kisheria).

Inadaiwa kuwa Julai 3 mwaka huu, mtoto mkubwa aliiba Sh. 150,000, fedha za mama yake mzazi na kwenda nazo shuleni kwa kuzificha kwenye mfuko wa madaftari yake.

Indaiwa kuwa kabla ya kufika shuleni, alibadili sare za shule na kuvaa gauni kisha kuondoka na mdogo wake kwenda Buhongwa.

Inaelezwa kuwa baada ya watoto hao kufika Buhongwa, waliomba wapangishwe kwenye nyumba ya Agnes Makonzele ambaye alikataa na akamtaka binti huyo awasiliane na mzazi wake. Binti huyo alianza kupiga simu kwa mama yake mzazi, akidai yeye pamoja na mdogo wake wametekwa huku akiomba watumiwe fedha ili watekaji wawaachie.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, alisema juzi jijini hapa kuwa jeshi lilipokea taarifa hiyo Julai 4 kutoka kwa Sarah Mzelengi (42), kuwa watoto wake wametekwa na watu wasiojulikana, wakidai watumiwe fedha ili waachiliwe.

Alisema kuwa baada ya taarifa hiyo, saa nane mchana siku hiyo, askari wa jeshi hilo walikwenda Mtaa wa Shibayi, wilayani Nyamagana ambako walipata watoto hao wakiwa wameomba hifadhi katika chumba cha nyumba inayomilikiwa na Agnes Magusu (57), anayoitumia kibiashara (anapangisha).

Alisema watoto hao walikutwa salama huku wakiwa na godoro moja la ukubwa mita tatu kwa sita, simu moja aina ya Cherry pamoja na vyombo vingine vipya vya matumizi ya ndani ambavyo vilinunuliwa na mtoto mkubwa (msichana) kwa kutumia fedha ambazo aliiba kwa mama yake mzazi.

Kufuatia tukio hilo, Kamanda Mutafungwa alikumbusha wazazi na walezi kuhakikisha wanaongeza malezi bora kwa watoto ili kuwaepusha na madhara wanayoweza kuyapata kwa kukosa usimamizi mzuri.



Mwenyekiti wa kijiji cha Loiborsoit, Kata ya Emboreet, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Lengai Ngulik akizungumza na wakazi wa kijiji hicho juzi, kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo sekta ya elimu na afya. **PICHA: GIFT THADEY**

# ‘Ujifunzaji unategemea macho kwa asilimia 80’

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI takwimu za ujifunzaji zikibainisha uwezo wa kuelewa kwa asilimia 80 unategemea macho, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) anafanya utafiti kujua ni kwa namna gani kundi la wenye ulemavu halipitwi na uelewa.

Mhadhiri Msaidizi UDSM, Raphael Mwambalaswa, mwenye ulemavu huo, anafanya utafiti huo ili kuja na majibu ya kukabiliana na changamoto kwa wenye ulemavu kama vile wasioona.

“Nimesoma machapisho na utafiti unaonesha asilimia 80 ya ujifunzaji hutegemea macho. Nikaamua kujikita katika eneo hili kwa kuwa na mimi nina ulemavu wa macho. “Nikajiuliza changamoto ni zipi kwa watoto wenye ulemavu wa kuona ambao hushindwa kufikia asilimia hiyo, wakiwa wanajifunza kama vile darasani? “Ninafanya eneo la ufundi mwenyewe kutengeneza madirisha ya alumium nikiwa VETA, kukamilisha Shahada ya Uzamivu (PhD),” alisema.

Mwalimu wa Ufundi Stadi na Mafunzo ya Uchomeleaji, Kintu Kiranga kutoka VETA, alisema chuo hicho hupokea makundi tofauti ya wanaohitaji kujifunza, ikiwamo watu wenye ulemavu wa aina tofauti.

Alisema Mwambalaswa ambaye ana ulemavu wa kuona, alifika chuoni kukamilisha PhD kwa kufanya ufundi, akitengeneza madirisha ya vioo. Alibainisha kuwa VETA kwa kipindi cha mwaka 2022/23 ilikuwa na wanafunzi wenye ulemavu 602.

# ‘RUWASA iziwezeshe kifedha na mafunzo jumuiya watumiaji maji’

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Godfrey Mnzava ameagiza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuweka utaratibu wa kuziwezesha kifedha na mafunzo Jumuiya za Watumiaji Maji ili zitunze vizuri rasilimali maji na miundombinu.

Aliagiza hayo jana wakati wa kuzindua mradi wa maji katika Kijiji cha Mabondeni, Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida ambao umegharimu Sh. milioni 280, ukitarajiwa kutoa huduma kwa zaidi ya wananchi 2,500.

Mnzava alisema serikali imekuwa inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kujenga miradi ya maji ili kuwezesha wananchi kupata huduma ya maji safi na salama, hivyo miundombinu ya miradi hiyo inapaswa kutunzwa vizuri ili iendelee kutoa huduma hizo na jukumu hilo linapaswa kufanywa na Jumuiya za Watumiaji Maji. Alisema wananchi pia wanapaswa kutunza vyanzo vya maji visiharibiwe kwa kuwa vyanzo hivyo vikiwapo vitaongeza upatikanaji maji na hivyo kuondoa kero kwa wananchi kama ilivyo dhamira ya serikali ya kusogeza huduma za maji kwa karibu kwa wananchi.

Mnzava ambaye aliridhia mradi huo na kuuzindua, alipongeza RUWASA kwa kutekeleza vyema mifumo ya ununuzi wa umma, hali ambayo imesaidia kupunguza malalamiko kwamba wapo baadhi ya makandarasi wanapendelewa kupewa zabuni za kujenga miradi ya maji.

Awali Meneja wa RUWASA Wilaya ya Manyoni, Gabriel Ngongi, akitoa taarifa ya mradi huo alisema mradi huo uliibuliwa na wananchi mwaka 2022 kwa nia ya kupunguza tatizo la ukosefu wa maji.

Alisema ujenzi wa mradi huo ulianza Agosti Mosi, 2023 na kukamilika Juni 15, 2024, ukijumuisha ujenzi wa kisima chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 4,000 kwa saa.

Ngongi alisema ujenzi wa mradi huo ulikadiriwa kutumia Sh. milioni 280.8, fedha kutoka Serikali Kuu kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (P4R), lakini hadi kukamilika kwake, umetumia Sh. milioni 275.88.

Alisema fedha hizo zimetumika kujenga ‘Pump House’, uunganishaji mfumo wa umeme, kununua na kufunga mitambo ya kusukuma maji, ujenzi wa mtandao wa bomba, ujenzi wa tangi la maji la lita 54,000 kwenye mnara wa mita 12 pamoja na ujenzi wa vituo vitano vya kutolea huduma ya maji.

Meneja huyo alisema faida za mradi huo ni pamoja na kuboresha kipato cha wananchi kwa kutumia muda mfupi wa kupata maji safi na salama kwa gharama nafuu na hivyo kutumia muda mwingi uliobakia kwenye shughuli za uzalishaji, kuboresha afya za wakazi wa Kijiji cha Mabondeni.

Faida nyingine ni kujenga mazingira mazuri ya wanafunzi kujisomea badala ya kutumia muda mwingi kutafuta maji atokapo shuleni na kupungua kwa kero kwa viongozi itokanayo na malalamiko ya kila siku ya ukosefu wa maji safi na salama.

“Sisi wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, hususani Kijiji cha Mabondeni kwa heshima kubwa tunashukuru serikali kwa kutuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu.

“Tumeona nia ya dhati ya serikali kumtua mama ndoo ya maji kichwani na tunaahidi kutunza mradi huu ili uendelee kuinufaisha jamii na kwa maendeleo endelevu,” alisema mmoja wa wakazi wa Itigi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali irejeshe mabilioni iliyochukua kutoka NHIF

**MFUKO** wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) uko hatarini kufisilika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anaripoti umepata hasara kwa miaka mitano mfululizo kutokana na kutoa zaidi ya unachoingiza.

Waajiri hawawasilishi kwa wakati michango ya wanachama wa mfuko; serikali haijalipa mabilioni iliyokopa katika mfuko; wastaafu wanalipiwa matibabu bila kuchangia huku magonjwa yasiyo ya kuambukiza yakigharimu mfuko mabilioni ya shilingi kila mwaka.

Kifungu cha 9 cha Sheria ya Mfuko huo kinawataka waajiri waliosajiliwa kuwasilisha michango inayodaiwa kwa mwezi husika ndani ya siku 30 baada ya mwisho wa mwezi.

Hata hivyo, inaporejewa Ripoti ya CAG kwa mwaka 2022/23 inabainisha jumla ya michango iliyokuwa inadaiwa hadi kufika tarehe 30 Juni 2023 ilikuwa Sh. bilioni 42.57.

Kati yake, michango ambayo inadaiwa taasisi za serikali ni Sh. bilioni 19.04 sawa na asilimia 45 na Sh. bilioni 23.53 sawa na asilimia 55 zinajumuisha madeni kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Uchambuzi zaidi wa CAG kuhusu hesabu za NHIF umebaini kuwa kati ya michango yote ya wanachama inayodaiwa na mfuko huo, michango ya Sh. bilioni 19.6 sawa na asilimia 40 inadaiwa zaidi ya siku 30.

Vilevile, mfuko ulikusanya Sh. bilioni 5.34 ya madeni hadi kufikia mwishoni mwa Novemba 2023 na kuacha deni linalodaiwa la Sh. bilioni 11.56.

Kwa mujibu wa CAG, sababu kuu zinazochangia madeni ya muda mrefu ya michango inayodaiwa kutoka mashirika ya umma, ni urasimu katika kuthibitisha madeni.

Madeni hayo ya muda mrefu pia yanasababisha changamoto za ukwasi katika mfuko, hivyo kuathiri shughuli za mfuko, ikiwa ni pamoja na kushindwa kuwalipa watoa huduma kwa wakati wanachama.

Nipashe Jumapili tunafahamu mambo makubwa manne yanayoathiri uhai wa muda mrefu wa NHIF, yakijumuisha mikopo ya serikali ambayo haijalipwa.

Kwa mujibu wa CAG, mikopo ambayo haijalipwa ni ya Sh. bilioni 208; inasababisha mzigo mkubwa wa kifedha, na hivyo kupunguza uwezo wa mfuko kuwekeza katika huduma muhimu na miundombinu.

Nipashe Jumapili tunafahamu, kama ilivyoripotiwa na CAG, serikali kupitia Wizara ya Fedha imepanga kulipa Sh. bilioni 180.03 (bila riba na adhabu) katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha (2024/25).

Jambo la pili linalonyooshewa kidole kuhatarisha uhai wa NHIF ni wastaafu kunufaika bila kuchangia, ikielezwa kuwa mfuko unagharamia matibabu ya wastaafu na wenza wao ambao hawachangii mfuko.

Ni hali ambayo inatajwa inadhoofisha mfuko kwa sababu matumizi ya wastani ya kundi hili ni Sh. bilioni 84.70 kwa mwaka.

Jambo la tatu ni kuongezeka magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanatajwa kudhoofisha mfuko kwa kiasi kikubwa kwa kuwa matumizi ya wastani kwa kundi hili hivi sasa ni ya wastani wa Sh. bilioni 137.80 kwa mwaka.

Tunafahamu pia kwamba kuna tatizo lingine la uchaguzi wa wanachama walio na wagonjwa, kwamba wanachama wa hiari kwa makundi fulani, hasa kutoka sekta binafsi zilizo rasmi na zisizo rasmi, hujiunga na mfuko pale tu wanapohitaji matibabu ya gharama kubwa, hali inayodhoofisha mfuko.

Nipashe tunafikiri ni muhimu uongozi wa NHIF ufikirie upya mikakati ya namna ya kuzalisha faida kutokana na kushughulika na wanachama na faida ya jumla kwa miaka mingi kwa uendelevu wa mfuko, lakini serikali ilipe mkopo inaodaiwa na mfuko huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii ielimishwe umuhimu wa PETS isaidie kudhibiti ulaji fedha za umma

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya vitu ambavyo baadhi ya wananchi huwa hawavitilii maanani, ni ufuatiliaji miradi au fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo katika maeneo hayo.

Wanafanya hivyo huku kukiwa na njia nyepesi na shirikishi wanayoweza kuitumia ili kujua matumizi ya rasilimali za umma kwa mfumo wa ufuatilia rasilimali za umma au PETS.

Mfumo huo kwa Kiingereza unaitwa Public Expenditure Tracking System (PETS), ambao unagusa maeneo matatu kuanzia mapato na matumizi taarifa na thamani ya fedha.

Kwa kawaida, mfumo huo unamtaka kila mwananchi awajibike kulinda rasilimali za nchi yake pia kufuatilia mapato na matumizi katika eneo lake kuanzia shuleni, kitongoji, kijiji, mtaa na kwingineko.

Hatua hiyo inamsaidia mwananchi kujua kama kuna fedha zimetolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji miradi, ajue ni kiasi gani cha fedha na jinsi itakavyotekelezwa.

PETS inaundwa katika mkutano mkuu wa kijiji au mtaa kwa ajili ya kufuatilia miradi inayoletwa na serikali ambayo imepewa kipaumbele na wananchi wa eneo husika.

Kamati ya PETS huanzia wajumbe sita hadi 15 wanaoweza kufuatilia mradi watakaoupa kipaumbele kufuatilia. Mfumo huo unasaidia kufanya viongozi wawajibike hasa kutokana na kujua kuwa kuna watu wanawafuatilia.

Baada ya kutoa ufafanuzi kidogo, ninarejea kwenye hoja yangu kuwa ipo haja wananchi wakaelimishwa kuhusu mfumo huo ili wawe na uelewa wa kutosha, wafuatilie miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Hilo lifanyike kwa sababu kumekuwapo tuhuma nyingi za utafunaji fedha umma au miradi kutekelezwa chini ya kiwango katika baadhi ya halmashauri nchini.

Kama nilivyoeleza awali, PETS inamtaka mwananchi kufuatilia mapato na matumizi, taarifa na thamani ya fedha ili kujua kama zitatumika ipasavyo au kama utekelezaji miradi unalingana na thamani ya fedha.

Ninadhani kuwapo kwa tuhuma za utafunaji wa fedha za umma au kutekeleza miradi chini ya kiwango kunachangia na wananchi kukosa elimu kuhusu mfumo huo, hivyo wanaona si wajibu wao kufuatilia.

Wakati mwingine inawezekana wale wanaoujua, wakawa wanakosa ushirikiano kutoka kwa viongozi, hasa kupata taarifa, lakini hicho kisiwe kikwazo, bali wachukue hatua kwenda ngazi nyingine kutoa taarifa.

Kwa kawaida kamati ya PETS haitakiwi kumshika mtu, wala kumpiga mtu, wala kumshtaki kama atakuwa amefanya hujuma, badala yake jukumu hilo ni la mkutano wa kijiji, huku kukiwa na kiongozi ambaye atakuwa ameitwa kusikiliza ubadhirifu ambao umefanywa.

Ninaamini kwamba wananchi wakielimishwa na kujua hatua hizo za PETS wa wajibu wao, inaweza kuwa rahisi kuwakabili wabadhirifu wa fedha za umma ili kuharakisha maendeleo.

Inasikitisha kuona serikali inatoa fedha kujenga madarasa na miundombinu mbalimbali ya shule, halafu inatekelezwa chini ya kiwango, huku baadhi ya fedha zikiishia mikononi mwa watu.

Vilevile, inasikitisha kuona serikali ikitoa fedha za ujenzi wa barabara katika maeneo mbalimbali nchini, halafu ujenzi unatekelezwa chini ya kiwango, huku wananchi wakiwa kimya kana kwamba hawapaswi kuhoji.

Hata Rais Samia Suluhu Hassan amewahi kusema viongozi na vyombo vingine havifanyi kazi ipasavyo katika wilaya, kitu ambacho kinasababisha ubadhirifu wa fedha za umma.

Ni wakati akihutubia katika mkutano wa hadhara katika Uwanja wa Majaliwa, wilayani Tandahimba, mkoani Mtwara, ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kikazi.

Kauli yake ilitokana na taarifa ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kuwa katika wilaya hiyo zimetolewa fedha za ujenzi wa vituo vya afya lakini haujakamilika.

Hivyo, wakati viongozi wakilala usingizi, ni vyema wananchi wasaidie kuwaamsha kwa kufuatilia kwa karibuni fedha au miradi ya maendeleo kupitia mfumo huo wa PETS, ili kuibua madudu.

# Miundombinu wezeshi kwenye urejelezaji itatatua kero ya taka

**Na Halfani Chusi**

TANZANIA inaweza kudhibiti na kufikia azma ya taka sifuri kwa kufanya urejelezaji na kuweka miundombinu wezeshi ya uchakataji taka.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi inayojihusisha na udhibiti wa taka nchini ya Nipe Fagio, Anna Rocha aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Miji ya Taka Sifuri uliokutanisha wadau mbalimbali.

Alisema kuwa hivi sasa Tanzania inafanya vizuri katika udhibiti wa taka kutokana na baadhi ya mikoa kuanza kutekeleza mfumo wa taka sifuri.

Alitaja mikoa hiyo kuwa ni pamoja na Arusha, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar, akisisitiza lengo la mkutano huo ni kujadiliana na kupeana elimu na namna ya kuifikisha katika mikoa mingine.

Alisema katika mkutano huo wawakilishi kutoka mikoa mingine nchini walikubali kupeleka elimu hiyo katika maeneo yao, ili kushirikiana kwa pamoja kudhibiti taka kama ilivyokuwa kwa Zanzibar ambao wamefanikiwa kupitia mfumo huo.

Alisema mfumo wa taka sifuri utasaidia kuifanya nchi kuwa safi, kuongeza ajira kwa vijana, kupata kipato kupitia faida zitakazopatikana kutokana na urejelezaji ikiwamo kuuza mbolea na chakula cha kuku.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Zanzibar, Mahmoud Mussa alisema utekelezaji mpango wa taka sifuri visiwani humo unalenga kuviweka safi visiwa hivyo.

Mratibu wa Miradi ya Ufadhili kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini nchini (TARURA), Humphrey Kanyenye aliitaka jamii kushiriki na kutekeleza lengo la taka sifuri lililowekwa.

"Tuna uwezo wa kupunguza taka kwa kutumia vikundi mbalimbali vilivyopo kwenye jamii zetu kwa kukusanya, kuchakata na kupata mbolea inayoweza kutumika katika kilimo, viwavi kwa ajili ya chakula cha kuku hivyo sisi kama TAMISEMI na TARURA wenye Miradi inayoendelea hasa katika Mkoa wa Dar es salaam ujuzi huu umetuongezea faida nyingine," alisema Kanyenye.

Alisema kuwa kupitia Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP) wameanza na Nipe Fagio na kwamba mpango waliona kwa sasa ni kuanzisha mfumo wa usimamizi wa taka ngumu.

"Hii njia wanayoitumia wenzetu wa mataifa mengine ni nzuri, na itatusaidia sana kutokana na elimu ambayo imetolewa pale Bonyokwa ni mfano mkubwa, wananchi wanakusanya taka na kuzigawa katika mafungu matatu kisha wanazilejeleza na zinazosalia wanazipeleka dampo.

"Mfumo wa taka sifuri unajumuisha kuzigawa katika makundi manne ambayo ni rejeshi, zile zinazooza, hatarishi na nyinginezo na kisha zinachakatwa na kurejelezwa kwa ajili ya kupata bidhaa mbalimbali kama vile mbolea na chakula cha kuku,"alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitazama mashinę ya mionzi CT Scan, kabla ya kuzindua huduma ya mionzi katika Hospitali ya Rufani ngazi ya Mkoa ya Tosamaganga, mkoani Iringa, jana. Wengine ni Askofu wa Jimbo Katoliki la Iringa, Mhashamu Tarcisus Ngalalekumtwa (kulia), Mkurugenzi wa hospital hiyo, Padri Benjamin Mafaume (wa tatu kushoto) na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba. **PICHA: OWM**

# Japan kuunganisha vipuri vya magari nchini

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) imesema wafanyabiashara kutoka Japan wanatarajia kuanza kuunganisha vipuri vya magari nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Latifa Khamis wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na Japan uliofanyika kwenye Viwanja vya Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), barabara ya Kilwa.

Mkurugenzi huyo alisema wafanyabiashara hao wameamua kuja kufunga vipuri vya magari nchini baada ya kuona Watanzania wengi wananunua magari Japan.

"Wamesema Watanzania tunanunua sana magari ya kwao, hivyo wameona kuna fursa na wanataka kuja kufungua kama sehemu ya 'shoe case' lakini kuunganisha vipuri vya hayo magari," alisema Latifa.

Katika mkutano wao huo uliokutanisha wafanyabiashara kutoka kampuni tisa za Japan na wafanyabiashara wa Tanzania, ukilenga kuangalia fursa zinazopatikana katika nchi hizo mbili, pia walikubaliana kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya miradi ya uwekezaji.

Kwa mujibu wa Latifa, maeneo mengine ya kuwekeza wanayoangalia ni katika sekta za kilimo, uvuvi, teknolojia, sekta za kutengeneza bidhaa za kuhifadhi vyakula na usafirishaji.

"Na kwa sababu wafanyabiashara hawa wote wanashiriki kwenye maonesho haya, tunataka baada ya hapa tufanye tathmini," alisema.

Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa, alisema majadiliano yaliyofanywa na wafanyabiashara wa nchi hizo mbili ni muhimu kwa kuwa yatasaidia kutoa mwelekeo mzuri wa kushirikiana kwenye uwekezaji.

Alisema amefurahia kushiriki katika mkutano huo wa kujadili na kuangalia fursa mbalimbali katika eneo la biashara na uwekezaji.

"Haya mataifa mawili ya Tanzania na Japan yamekuwa yakishirikiana kwa kipindi kirefu na sasa tumeona tuje tujadiliane namna ya kuongeza nguvu zaidi kwenye sekta za uzalishaji, kwahiyo tumebadilishana uzoefu wa kibiashara.

"Historia ya nchi hizi katika ushirikiano inatupa moyo kuendelea kushirikiana zaidi katika maeneo muhimu hususani ya kukuza uchumi," alisema Misawa.

# Mfumo e-Mrejesho waipa Tanzania tuzo ya kimataifa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema ushindi wa tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 'UN Public Service Innovation Awards' kupitia mfumo wa e-Mrejesho ni kielelezo cha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

Mfumo huo umetambuliwa na umoja huo kama jukwaa linalowezesha serikali kukusanya maoni na malalamiko ya wananchi kwa njia ya kidijitali na hivyo kufanya uamuzi wa sera na utekelezaji kwa wakati.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilifanyika Juni 26 mwaka huu, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa 'UN Public Service Week 2024' katika Jiji la Incheon, Jamhuri ya Korea.

Tanzania ilikuwa moja ya nchi mbili tu za Afrika zilizotunukiwa tuzo hiyo, nyingine ikiwa ni Afrika Kusini ambapo jumla ya nchi 73 wanachama wa Umoja wa Mataifa zilishiriki na mifumo 400 iliwasilishwa wakati mifumo 15 pekee ndiyo ilishinda tuzo mbalimbali ukiwamo mfumo wa e-Mrejesho.

Tuzo hizo zilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Idara ya Masuala ya Kiuchumi na ya Kijamii, Li Junhua, pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Korea, Lee Sang-min, na kupokewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba, alisema kuwa tuzo hiyo inaonesha utambuzi wa mchango mkubwa wa mfumo wa e-Mrejesho duniani kama jukwaa huru linalounganisha wananchi na serikali katika kuboresha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

Alisema mfumo huo unaruhusu serikali kukusanya malalamiko, maswali na maoni ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa wakati na pia, unamwezesha mwananchi kutuma maoni yake bila kujulikana ikiwa mwananchi hatotaka kujulikana.

"Mfumo wa e-Mrejesho ni jukwaa huru kwani umezingatia faragha za wananchi ambapo kwa wale wasiopenda kujulikana wanapowasilisha maoni yao serikalini wanaweza kuwasilisha bila kujulikana, na hivyo kuhakikisha sauti za watu zote zinasikilizwa, hii inachochea utamaduni wa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma," alisema.

Ndomba alisema mfumo wa e-Mrejesho ni hatua kubwa katika juhudi za e-GA za kujenga daraja kati ya serikali na wananchi.

Alisema ushindi wa tuzo hiyo unaonesha azma ya e-GA ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala wa umma kupitia teknolojia inavyotekelezwa.

Alibainisha kuwa ikiwa mwananchi atakosea kuwasilisha malalamiko yake katika taasisi husika, mfumo wa e-Mrejesho unaruhusu kuyahamisha kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine.

Pia alisema unamruhusu mwananchi kukata rufani kwenda ngazi ya juu ya taasisi ikiwa hatoridhika na majibu yaliyotolewa kuhusu alicholalamikia.

"Mfumo huu unasaidia kuongeza uwajibikaji, kwani lalamiko linapofika kwenye taasisi litaonekana ngazi zote za uongozi wa taasisi hiyo na kila ofisa aliyelifungua ama kulifanyia kazi ataonekana," alisema.

Pia alisema unafanya uchambuzi wa taarifa na kumwezesha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Utumishi na Katibu Mkuu Kiongozi kuona malalamiko yaliyo wazi, yanayoshugulikiwa na yaliyokamilika kupitia 'dashboard' maalum," alisema Ndomba.

Machi 13 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwataka viongozi wa umma kutumia Mfumo e-Mrejesho ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu serikali na kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo ili kuimarisha uwajibikaji kwa viongozi wa umma.

Wiki ya Huduma ya Umma ya Umoja wa Mataifa ni tukio la kila mwaka linaloadhimishwa kimataifa kwa lengo la kusherehekea thamani na umuhimu wa huduma ya umma kwa jamii na hujadili jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma kwa umma duniani kote.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Maofisa wa Idara ya Uhamiaji, walioteuliwa na Rais, wakila kiapo cha uadilifu katika utumishi wa umma, baada ya kuapishwa na Kamishna Jenerali Uhamiaji, Dk. Anna Makakala (hayupo pichani), kabla ya kuanza Kikao Kazi, jijini Dar es Salaam juzi. Kutoka (kushoto) ni Naibu Kamishna, Mohamed Awesu Bakari, Naibu Kamishna, Gharib Ali Yusuf, Naibu Kamishna Kigongo Mashauri Shile na Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Dismas Josephat Mosha. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Bingwa wa Upasuaji, Kinywa, Meno na Uso, Dk. Gemma Berege (kushoto), akizungumza na mmoja wa wananchi aliyefika katika Banda la Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), katika maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), kwenye uwanja wa Mwalimu Nyerere, barabara Kilwa juzi. Wengine ni maofisa wa hospitali hiyo. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa barabara ya Karutah, mjini Bariadi jana, kwa kiwango cha lami. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Manyara, Regina Ndege (kushoto), akizungumza na viongozi wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), wilaya ya Kiteto, kuhusu kushiriki kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, wakati wa mkutano uliofanyika katika Kata ya Kibaya, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**



Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Firimin Msiangi (kulia), akizungumza jambo wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo cha nyaraka na kumbukumbu za Muungano (Makavazi), katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mtumba jijini Dodoma juzi. Katikati ni Mkurugenzi Msaidizi (Sera, Utafiti na Ubunifu) Ofisi ya Makamu wa Rais, Paulo Laizer na Kaimu Mkurugenzi wa Muungano, Hanifa Selengu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MAISHA

JULAI 7, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 13



## UNATAKA KUMPA GAWISHA?



## NYUMBANI:

Acha kuokoteza ramani ya nyumba



Ukurasa 12

## HARUSI



# CHONGA PUA

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 24 | 25 | 26 | | | 10 | 11 | 12 |
| 71 | 72 | 73 | | | 51 | 52 | 53 |
| 42 | 43 | 44 | | | 31 | 32 | 33 |
| 15 | 16 | 17 | | | 19 | 20 | 21 |
| 89 | 90 | 91 | | | 66 | 67 | 68 |
| 57 | 58 | 59 | | | 87 | 88 | 89 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | | S | I | A | S | A |
| H | | | | K | | C |
| A | | I | L | I | | H |
| N | T | A | | L | O | A |
| G | | M | E | I | | N |
| W | | K | | | | G |
| E | L | E | Z | A | | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


BAA, NIA, SAA, NOA, AMANA, KILWA, LOANA, BANDA, ANGALIA, ONESHEA

## TOA TOFAUTI 5





## AMSHA AKILI

KATI YA HERUFI A, B NA C NI IPI INAWEZA KUIFIKIA HERUFI Z? TAFUTA NJIA




## PAKA RANGI




### Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Penzi la kweli halionekani kwa macho!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kujadili maisha yalivyo katika jamii na familia zetu. Maisha ni mchakato pia mapambano. Mwanadamu kubadilisha mawazo ni jambo la dakika kama si sekunde.

Wakati mwingine mazingira aliyoko yanaweza kumbadili mawazo au fikra fulani au kufutilia mbali mipango fulani na kuamua vinginevyo. Yapo mambo mengi yanayochangia hali hiyo kutokea.

Leo tujadili wale wanaokwenda kufunga ndoa kinyemela wanapokuwa masomoni Ulaya. Kabla sijaendelea, hebu tusikie email ya msomaji wetu huko majuu akitolea mfano anachokishuhudia huko.

Anti, nimeifuatilia vizuri stori iliyowahi kuchapishwa kwenye safu yako kuhusu ndoa halali na ndoa zile zisizo halali.

Kwa ujumla, tutambue kuwa kuna utofauti mkubwa kati ya ndoa, familia na urafiki ambavyo vyote vimebebwa na kitu mapenzi. Hakuna asiyejua maana ya ndoa, hali kadhalika familia. Urafiki ndio hatua ambayo huvuruga ndoa na familia.

Fikiria umepata nafasi kwenda kusoma nje ya nchi na tayari umeolewa au kuoa. Ghafla unakutana na rafiki wa zamani. Tambua kuwa rafiki uliyempata hajaoa au kuolewa ila wewe umeacha mwenzako Tanzania na ukumbuke kuwa masomo yatachukua miaka minne.

Hatimaye katika hili na lile mmepata kazi ya muda wa ziada ambayo mnaifanya baada ya masomo mkiwa huko ughaibuni. Ulianza kama urafiki lakini mwishowe mkawa wapenzi.

Ndoa iko wapi? Familia iko wapi? Wawili hawa wanasahau yaliyopita wanaanza ukurasa mpya wa maisha. Ni vigumu sana kutambua kilicho ndani ya moyo wa mwenzio, na kusema ukweli, penzi la kweli halionekani kwa macho na ukiliona huwa tayari limepita. (Pascal David Karachi, Pakistan).

Naam. Kumbe jamaa zetu wengine wakipata mwanya wa kwenda kusoma huko, huacha mbachao kwa msala upitao? Au ndiyo yaleyale tunayoambiwa kwenye ule msemo mwingine kuwa fimbo ya mbali haiui nyoka?

Msomaji wetu, Pascal amesema 'penzi la kweli halionekani kwa macho'. Hizi ni hisia zinazotoka moyoni mwa mtu. Labda ubahatishe kutambua kile akiwazacho mtu, lakini huwa ni siri moyoni labda ukijue kupitia matendo yake au akitamkacho kwani ndicho kilichoujaza moyo wake.

Ni kweli baadhi ya watu waliokwenda kusaka kipato nje ya nchi au masomoni, lakini huko wakaanzisha uhusiano mpya, japokuwa nyumbani tayari walikuwa na familia. Wapo walioweza kukuta nyumba zao salama na wengine zimebomoka baada ya taarifa kuthibitishwa.

Tatizo ni wale tayari wana familia. Lakini kwa wale ambao wanakuwa wasela, iwe ni mwanamke au mwanamume, wao kwenda kuanzisha uhusiano wa kimapenzi Ulaya, Asia na Amerika haiwasumbui. Na wapo waliojikuta wakilowea huko baada ya masomo na wengine kurejea na wachumba au ndoa zilizofungiwa hukohuko.

Kwa wale ambao huvunja mwiko wakati tayari wana familia nyumbani, ndio wale kama ni mwanamume aliacha mke nyumbani, hukuta mkewe huyo amehama nyumbani au anasubiri ushauri wa kifamilia baada ya kupata taarifa kuwa mumewe ana mke wa Ulaya.

Lakini wakati mwingine wanaokwenda huko majuu wakati wana familia zao, utawasikia wakitamba kuwa hawawezi kutazama wazuri Ulaya na kumeza mate tu. Au wanasema maadam familia nyumbani iko vizuri haina shida, kwanini naye asijinafasi na vidosho au vibosile kupoteza muda hadi arejee nyumbani. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Kwa ujumla, uhusiano wa kimapenzi umeficha siri kubwa sana. Ninapenda nirudie kusema kuwa si rahisi kujua anachokiwaza mtu moyoni mwake.

Ni kama vile mwenzako anakuaga kwamba niko jirani ninapata kinywaji kumbe ameshafika umbali wa zaidi ya kilomita tano kumfuata mchuchu wake. Kama mkewe angejua anakwenda umbali ule tena kufuata nyumba ndogo yake, ugomvi huo ungeisha leo?

Anayowaza mtu ni sawa na usiku wa giza. Hana tofauti na mtu anayepanga mauaji na kwa siri akayatekeleza bila kugundulika. Lakini husahau kuwa hata kama hakuna mwanadamu aliyemwona, yupo mkuu wa yote, Mungu wa mbinguni anayeona vinavyoonekana na visivyoonekana.

Imani inaleta faraja kubwa sana na ukiishikilia, Mwenyezi Mungu ana uwezo mkubwa wa kukusimamia na kukuepusha kwa mabaya yote yaliyolenga kukuumiza. Unapokwenda majuu kuwa makini na zaidi zingatia kilichokupeleka ili kujiepusha na migogoro katika maisha yako.

**Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Ujumbe 0715268581. Namba hii ipo WhatsApp. Email: fwingia@gmail.com**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Wabunge wetu kuna la kujifunza maandamano ya Gen Z Kenya

MPAKA sasa sidhani kama kuna mtu anayemjua mwasisi wa Gen Z (vijana wa kizazi kipya) kule Kenya. Ndio maana kuyazima maandamano hayo ya umma imekuwa shughuli pevu.

Hakuna anayejua vizuri chimbuko halisi la vijana hao wanaoandamana. Lakini, Gen Z ni kundi rika lenye kuhusisha watu waliozaliwa kuanzia mwaka 1996 mpaka 2010.

Mwenye umri mkubwa zaidi katika kundi la Gen Z ana miaka 28 na mdogo kabisa ana umri wa miaka 14. Wakati mwingine Gen Z, huitwa Zoomers.

Gen Z ni watoto wa makundi rika ya mwisho wa karne ya 20. Ni kundi rika lenye uelekeo wa kuongoza makundi mengine duniani katika miaka mitano ijayo.

Mei 24, 2024, kule kwa majirani zetu Kenya, Muswada wa Fedha uliwasilishwa bungeni kwa mara ya kwanza, ukiwa na kurasa tano, ndio uliosukuma vijana wadogo wa Generation Z kuingia barabarani kuupinga.

Hoja yao ni kwamba, ukitiwa saini na Rais William Ruto kuwa sheria kamili, utazidi kufanya maisha kuwa magumu.

Muswada huo pamoja na mambo mengine umebeba nyongeza ya kodi na ushuru. Hii inajumuisha asilimia 1.5 ya kodi ya kidijiti kwa majukwaa ya ndani yenye kutoa huduma kama ajira kwa njia ya intaneti, ukodishaji, uuzaji chakula na usafiri.

Kuna hofu kubwa kuhusu ugumu wa maisha. Kwamba, gharama za maisha zipo juu, hivyo vijana wa Gen Z wanaona kodi zikiachwa hivyo, zitaumiza vijana wengi.

Baada ya serikali ya Rais Ruto kukubaliana na hoja za vijana wadogo wa Generation Z, aliamua kutotia saini muswada huo, akiahidi kurejesha bungeni.

Lakini akasisitiza kwamba kutokana na kutotia saini muswada huu ili kutuliza munkari wa vijana hao, alisema serikali yake italazimika kukopa matrilioni ya shilingi ili kujiendesha.

Julai 5, 2024, Rais Ruto alizungumza na Gen Z kupitia mtandano wa kijamii wa X. Katika hotuba yake, Rais Ruto alizungumzia baadhi ya masuala, ukiwamo uamuzi wa serikali yake kubana matumizi.

Akaenda mbali zaidi akisema, serikali yake itasaidia familia ambazo vijana wao waliuawa katika maandamano.

Vilevile, alisema serikali yake imeunda kikosi kazi cha kufanya uchunguzi wa Deni halisi la Serikali na kushauri hatua za kuchukua.

Wabunge wetu wa Tanzania kuna la kujifunza hapa. Hebu jiulizeni kuna mambo mangapi yanaumiza? Wenzenu huko Kenya wamepata somo kuhusu miswada wanayoipitisha kwamba wanapaswa kuitafakari kwa kina kabla ya kuipitisha.

Hakuna shaka kwamba maandanao ya Gen Z yameisukuma serikali ya Rais Ruto kupendekeza Bunge lao lipunguze Sh. trilioni 3.66 katika bajeti yake.

Siyo hayo tu ya kujifunza kwa Wakenya. Angalia Rais Ruto, anasema washauri wa Ikulu katika serikali yake wamepunguzwa kwa asilimia 50 ili kubana matumizi.

Hata ununuzi wa magari mapya ya serikali yao umesitishwa kwa miezi 12, isipokuwa kwa magari ya usalama.

Hapohapo, serikali hiyo ya Ruto imelazimika kufikia uamuzi wa kuwataka watumishi wa umma waliofikisha umri wa miaka 60 kustaafu haraka.

Hili lina maana kubwa sana na ni funzo kwa serikali nyingine za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC).

Rais Ruto ametangaza serikali yake imeamua kufanya maboresho katika vipaumbele vyake, ikiwamo kupunguza matumizi katika taasisi zake.

> **"Baada ya serikali ya Rais Ruto kukubaliana na hoja za vijana wadogo wa Generation Z, aliamua kutotia saini muswada huo, akiahidi kuurejesha bungeni.**

Na pia serikali yake imeamua kuondoa vipaumbele vyake, kufuta uteuzi wa makatibu tawala na kufuta idara 47 ambazo hazina uzalishaji.

Nilitamani kuwaona namna mlivyolibeba suala la kuongezeka kwa tozo ya Sh. 500 katika ununuzi wa umeme kupitia Luku.

Hata ule mgomo wa wafanyabiashara kufunga maduka kupinga sheria za kodi ambazo wafanyabiashara hawakutaka kuzitaja.

Nani ambaye hakuona mgomo huo ulivyotikisa kwa siku tatu hadi nne katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro (Moshi Mjini) na Njombe?

Ninamuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kubadili uongozi wa Wizara ya Viwanda na Biashara, pia Mamlaka ya Mapato (TRA), pengine ni kutuliza yaliyojitokeza.

Bravo kwa serikali ya Tanzania kwa hilo. Sasa wabunge wetu mmejifunza chochote huko Kenya?

***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI





Baada ya miaka mitatu ya ndoa, Ramadhan Mashkando na mkewe imekuwa kumbukumbu nzuri kwa siku kama hii muhimu kwao. Tunawatakia maisha mema na yenye furaha.





MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# UNATAKA KUMPAGAWISHA?

JE unataka kumpagawisha mpenzi wako ambaye unataka kuonana naye kwa mara ya kwanza? Basi unaambiwa mavazi ni moja ya kivutio kinachomfanya mpenzi wako afe kimahaba kabla hamjazungumza.

Kitu muhimu katika siku ya kwanza lazima ujihakikishie unapendeza kiasi cha kila mtu akuone upo tofauti.

Siku hiyo muhimu hakikisha unampa mshtuko pale anapokuona kwa jinsi ulivyopangilia nguo na kuonekana kama umeshuka kutoka mbinguni.

Nguo inayopendeza zaidi ni rangi nyekundi ambayo inaleta maana upendo katika mapenzi.

Unaweza kuchanganya nguo za floral, ambazo licha ya kuonekana ya kifahari, inaonyesha ujasiri na kujiamini kwa mwanamke

Ukimaliza hapo tupia kitu chochote chenye waridi ya dhahabu. Rangi hiyo inavutia na lazima utamkamata na hawezi kutikisika.

Weka vikorombwezo vingine kama rangi ya kucha nyekundu, pochi la mkononi,viatu, mkanda, au ua jekundu kichwani.

Ukitaka kumpagawisha zaidi, vaa suruali ya jeans iliyobana na top nzuri ya rangi nyekundu inayoshika vizuri mwili.

Vazi hilo linaendana na viatu virefu ambavyo utavimudu kutembea vyema katika mwendo wa paka.



## UREMBO
Na Mary Geofrey

# CHONGA PUA

UTUMIAJI wa vipodozi maarufu kama 'MAKE-UP' inawezesha kubadili kwa kiasi kikubwa taswira ya mtu na kumfanya kuwa tofauti.

Haishangazi kuona wataalamu wa kujipodoa kufanya maajabu kwenye uso wako na wakati ukajisahau kama ndiyo mwenyewe.

Kuna vidokezo kadhaa ambavyo hutumika kutengeneza pua ili kuwa katika mwonekano mwembamba na wa kuvutia.

Kufanya pua yako ionekane ndogo ni suala tu la mbinu kadhaa za kutengeneza kwa ubunifu.

Ikiwa unataka pua yako ionekane nyembamba tumia 'foundation' kwenye pembe za nje za pua yako.

Foundation lazima uwe na vivuli viwili vyeusi kuliko sauti yako ya ngozi ya asili.

Baada ya haya, weka foundation nyepesi katika vivuli viwili kwenye daraja la pua yako.

**Tumia bronzer**

Paka bronzer kwenye paji la uso wako, kidevu, mashavu, na chini ya katikati ya pua yako. Hii itafanya pua yako ionekane nyembamba na ndogo. Bronzer itaongeza asili kwa ngozi yako.

**Pua ndefu**

Unaweza kufanya pua yako kubwa ionekane ndogo kwa kutumia foundation. Paka rangi nyeusi ya foundation kwenye ncha ya pua yako na kati.


Changanya vizuri ili iweze kuonekana asilia.

**Chini ya Macho**

Miduara ya giza chini ya macho yako itaunda kivuli na hiyo itafanya pua yako ionekane kubwa zaidi.

Daima tumia kificho kufunika miduara ya giza na itafanya pua yako ionekane nyembamba.





## MAPISHI
Na Mary Geofrey





# Vileja vya Tambi

VILEJA ni aina ya vitafunwa ambavyo mara nyingi hupendelea kuliwa na familia, lakini kupika wengi hawafahamu.

**Mahitaji**

Tambi nyembamba mifuko miwili, siagi vijiko vya supu vinne, maziwa ya sona 300Ml zabibu kavu kikombe kimoja, arki (vannila) Kijiko cha supu kimoja.

**Jinsi ya kupika**

Weka karai au sufuria kwenye moto kiasi tia siagi, weka tambi uzikaange usiachie mkoni mpaka ziwe rangi ya dhahabu.

Kisha weka zabibu huku unakoroga, weka maziwa na huku unakoroga usiachie mkono na weka arki.

Epua karai, tumia kijiko cha chai kwa kuchotea na utie kwenye kikombe cha kahawa nusu usikijaze.

Kipindue kwenye sahani utoe kileja na acha kwa dakika 10 vitakuwa tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# ACHA KUOKOTEZA RAMANI YA NYUMBA

UJENZI wa nyumba hauwezi kufanyika pasi na ramani inayoonesha dira ya aina ya nyumba inayotakiwa kujengwa.

Pamoja na kutakiwa kuwapo ramani kabla ujenzi wa nyumba, wapo baadhi ambao wamekuwa hawalichukulii kwa umakini suala la kuwa na ramani kutoka kwa wataalamu wanaoeleweka na badala yake 'kuokoteza' tu.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Lameck Kashabo, anasema kuokoteza ramani na kutokuthamini kile unachokwenda kujenga licha ya kwamba unatumia mamilioni ya shilingi kujenga ni hatari na mwisho wake huwa majuto.

"Inashangaza sana kwamba unakuta mtu anakwenda kujenga nyumba ya Sh. milioni 90 lakini anaokoteza ramani kutoka kwa wasio wataalamu au anatafuta ramani ambayo imetumiwa na mtu mwingine wakati gharama ya kumtumia mtaalamu kwa huduma yote ya ushauri pamoja na michoro labda ni Sh. 600,000 ambayo haifiki hata asilimia moja ya gharama yote ya ujenzi. Uamuzi wa aina hii kwa vyovyote vile unaambatana na hasara kubwa na majuto ya baadaye," "Madhara ya kuokoteza ramani ya nyumba kisha ukaijenga, iwe ni kutoka kwenye mitandao au ni kutoka kwa mafundi wa mitaani au kwa namna nyingine yoyote ile ni kushindwa kuthamini nyumba unayotaka kujenga licha ya kwamba unakwenda kutumia fedha nyingi sana kuijenga," anaonya Kashabo.

Anasema miongoni mwa madhara ya kuokoteza ramani ni kushindwa kupata aina ya nyumba unayotaka kwa kulazimika kukubaliana na chochote unachokutana nacho kwenye ramani unayookoteza.

"Kila mtu huwa na vipaumbele tofauti na vya mwingine, karibu kila kazi tunayokutana nayo huwa ni vigumu kufanana na ya mtu mwingine kwa vipaumbele vya kimahitaji, achilia mbali utofauti wa ukubwa wa viwanja, utamaduni na mengineyo, na ndiyo maana huwa ninawashauri watu kufanya kitu kinachoendana na vipaumbele vyao.

"Huwezi kufurahia nyumba ambayo si chaguo lako, hata kama ikitokea ukapenda aina fulani ya jengo au nyumba kutokana na muundo wake, bado kwa ndani kuna vitu hutavifurahia namna jinsi vilivyopangika hivyo unachotakiwa ni kuchukua picha ya lile jengo ulilolipenda na kisha kumwonyesha mtaalamu, kumwambia kwamba 'ninataka liwe na mwonekano huu' lakini ukamwelekeza alipangilie upya kwa ndani na mwisho wa siku libaki na mwonekano ule unaoupenda wewe.

"Unaweza kujuta sana baadaye unapookoteza ramani, kisha ikajengwa kama ilivyo au hata kama itabadilishwa ikawa kienyeji sana na hata usiipende tena. Bila kutumia utaalamu sahihi mara nyingi changamoto zake unakuja kukutana nazo baada ya kuanza kuitumia," anasema mtaalamu huyo.



# Kibaraza kinachopendeza

Na Restuta James

MAUA halisi, pambo la asili ukutani, viti vichache na meza ndogo nzuri ni vitu vitakavyokupa hamu ya kukaa katika kibaraza chako.

Wataalamu wa mapambo wanaeleza kwamba hivi ni vitu vinavyonogesha mandhari ya kibaraza, kiwe kikubwa au kidogo.

Baadhi ya wataalamu kwenye mtandao wa Pinterest, wanasema matumizi ya vitu vya asili katika eneo hilo yakiwamo maua kunaongeza hewa na utulivu.

Wanasema 'visosi' au nyungo vilivyofumwa kwa ukili na kunakshiwa kwa rangi tulivu ni pambo tosha kibarazani.


"Panapendeza sana ukiweka meza ndogo ya mbao, unaweza kujenga mazoea ya kunywa kahawa kibarazani au kupumzika ukisoma kitabu cha riwaya au jarida ulipendalo," anasema mtaalamu Ryan Peter.

Anasema kwa wanaopenda kukaa chini, wanaweza kuweka mkeka au zulia kulingana na uwezo wa mtu.


Anashauri kuwa kibaraza ni eneo linalohitaji kuwekwa vitu vichache na hasa maua ili liweze kuleta utulivu.

"Unaweza kuweka stand ya kubeba makopo matatu au manne ya maua na kama ni eneo kubwa lenye kona, unaweza kuweka stand mbili za aina hiyo. Maua yawe yanayochanua meupe au pinki ili upate utulivu. Ukiweka yanayochanua rangi nyingi hutokifurahi sana," anafafanua.

Kwa nyakati za jioni, anashauri kuwasha mishumaa miwili au isiyozidi mitano, ili kuweka mwanga.



# KATUNI


KATUNIKA
KI'DOMOKRA
2014
Na ABDUL KINGO
JUKWAANI
MPAKA NAUZIWA KIWANJA HUKU SIJUI NILIKUJA BILA MACHO?!
BABA SI ULISEMA ULINUNUA UKIWA UMELEWA CHAKALI?
TENA SIKU HIYO "NILIZITANDIKA" TOKA ASUBUHI NIKAJA JIONI
ULIAMBIWAJE ULIPOKUTANA NA DALALI?
NNA BAHATI KUPATA KIWANJA BAHARINI
KWELI BAHATI
USITAKE KUNAMBIA HAYA NNAYOYAONA YANA UKWELI!
WAMEHAMA "MAHOTELINI" WAPO GESTI!
KESI UMESHINDWA KWANINI UMLEE?
UTARUDISHA MILIONI YANGU AU NIACHILIE HII KOKI?
JANAMKE KIHEREHERE SIJAPATA KUONA!
DEREVA USITULETEE WAZIMU KUTAKA KUTUUA! SISI BADO TUNAUPENDA UGALI.
SI MLIKUWA MNASEMA MNA-PENDA KWENDA PEPONI?
KWA HIYO WEWE NI WAKALA WA ZIRAILI?
SHIKAMOO MZEE... WEWE NI MKARIMU MCHESHI, MPENDA WATU, MSOMI PIA HUNA MAJIVUNO...!
KODI YANGU KWANZA!... ALAFU HUO WASIFU WA 'MAREHEMU' BAADAE.
UNALALAMIKIWA "UKILA MONDE" UNAACHIA "KUBWA" VICHOCHORONI
WAMEZOEA KUPUNJWA! BASI NITAKUWA NAWA-ACHIA NDOGO.

HABARI KIMATAIFA

# Pezeshkian ashinda urais Iran

**TEHRAN,** IRAN

MGOMBEA wa urais mwenye msimamo wa wastani nchini Iran, Masoud Pezeshkian, ameshinda katika uchaguzi uliofanyika kwa mara ya pili.

Pezeshkian alimshinda mpinzani wake Saeed Jalili, mwenye msimamo mkali kwa zaidi ya kura milioni tatu. Mwanasiasa huyo anayeegemea katika siasa za mageuzi alishinda uchaguzi huo ambao ulionekana kuwa na ushindani mkali baada ya duru ya kwanza kushindwa kupata mshindi.

Matokeo hayo yaliyotangazwa na Wizara ya mambo ya ndani yanaonyesha kuwa Pezeshkian, alipata zaidi ya kura milioni 16 na Jalili alipata milioni 13, kati ya kura milioni 30 zilizopigwa.

Msemaji wa mamlaka ya uchaguzi Mohsen Eslami alisema watu waliojitokeza kupiga kura ilifikia asimilia 49.8.. Viongozi mbalimbali duniani akiwemo Rais wa Russia, Vladmir Putin na uongozi wa Saudi Arabia wametuma salamu za pongezi kwa mwanamageuzi huyo kwa kuchaguliwa kuwa rais wa Iran. Masoud Pezeshkian ameutumia mtandao wa X, kuwashukuru watu wa Iran kwa kumchagua. Itakumbukuwa kuwa uchaguzi huo, uliitishwa baada ya kifo cha aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Ebrahim Raisi, katika ajali ya helikopta.

**DW**



Wakimbizi wa Sudan wakiwa kambini katika jimbo la Gedaref mashariki mwa Sudan hivi karibuni. **PICHA: AFP**

# Viongozi wa kijeshi wakutana Niger

**NIAMEY,** NIGER

VIONGOZI wa kijeshi kutoka nchio tatu za Afrika Magharibi, wamekutana kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kuunda umoja wao.

Kiongozi wa Niger, Jenerali wa Niger Abdourahamane Tchiani , jana alimpokea Kapteni Ibrahim Traoré, kiongozi wa Burkina Faso, aliyekwenda kuhudhuria mkutano huo. Viongozi hao wa serikali tatu za kijeshi za Afrika Magharibi, Burkina Faso, Niger na Mali wanatarajiwa kukutana ili kuimarisha muungano uliofundwa baada ya kujiondoa uwanachama wa jumuiya ya kiuchumi ya Ecowas.

Wanajeshi hao walichukua madaraka katika mfululizo wa mapinduzi kutoka 2020 hadi 2023.

Nchi hizo zinaunda Muungano wa Mataifa ya Sahel. Mataifa hayo yameathiriwa na ghasia za wanamgambo wa jihadi.

Viongozi hao walitangaza mpango wa kuondoka katika Ecowas, ambayo inafanya mkutano wake kilele siku ya Jumapili.

Katika mkutano unaofanyika katika mji mkuu wa Niger, Niamey, wakuu hao wa serikali za kijeshi wanatarajiwa kuanzisha rasmi muungano huo, unaojulikana kwa kifupi kwa lugha ya Kifaransa kama AES.

Nchi zote tatu ziliwafukuza wanajeshi wa Ufaransa waliokuwa kama sehemu ya ujumbe wa kupambana na jihadi na kuigeukia Russia kama nchi rafiki.

**BBC**

# Wanajeshi 27 wahukumiwa kifo DRC

**GOMA,** DRC

WANAJESHI wawili wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wamehukumiwa adhabu ya kifo baada ya kupatikana na hatia ya kukimbia vitani wakati wa mapigano.

Hukumu hiyo imetolewa siku tatu baada ya wanajeshi wengine 25, kuhukumiwa adhabu kama hiyo.

Kesi hiyo imefanyika wakati waasi wa M23, wanoungwa mkono na Rwanda, wanashikilia maeneo mengi baada ya kuyateka kutoka mikononi mwa jeshi la serikali wiki iliyopita.

Hata hivyo, mapigano yanayoendelea katika mkoa wa Kivu Kaskazini.

Tangu mwishoni mwa mwaka 2021, waasi hao wamedhibiti maeneo mengi katika mkoa huo, karibu na mji mkuu wake wa Goma.

Hata hivyo, upande wa utetezi ulipinga hukumu hiyo na kutangaza nia yake ya kukata rufaa kama ilivyokuwa siku ya Jumatano wakati askari 25 walipohukumiwa kifo katika kesi iliyosikilizwa katika kijiji cha Alimbongo.

Askari wengine wanane walihukumiwa kifo katika eneo la Goma mwezi Mei kwa kosa la kukimbia adui.

Takriban askari thelathini, wakiwemo makapteni wasiopungua watatu, wamehukumiwa kwa makosa ya uoga, kukimbia adui, kutawanya mabomu ya kivita, ukiukaji wa maagizo, mauaji, wizi na unyang'anyi.

Wanajeshi wengine wanaoshtakiwa walitarajiwa kupandishwa kizimbani jana..

Serikali ya DRC iliamua kuondoa sheria ya kusitisha utekelezaji wa adhabu ya kifo ambayo imekuwa ikitekelezwa kwa zaidi ya miaka 20.

## Hamas wakubali kusitisha vita

**GAZA,** PALESTINA

KUNDI la Hamas imekubali pendekezo la Marekani la kuanza mazungumzo ya kusitisha vita pamoja na kuachiliwa kwa mateka wa Israel.

Ofisa mkuu wa kundi hilo alisema tayari wamefikia muafaka baada ya kutafakari kwa kina kuhusu pendekezo hilo.

Hata hivyo, hamas imeitaka Israel iahidi kusitisha mapigano ya kudumu kabla ya wao kusaini makubaliano hayo ambayo yangeruhusu mazungumzo ya kipindi cha wiki sita, chanzo hicho kiliaambia shirika la habari la REUTERS.

Ofisa mmoja wa Palestina aliye karibu katika juhudi za kutafuta amani alisema pendekezo hilo linaweza kupelekea kufikiwa muafaka iwapo Israel italipitisha na itamaliza vita hivyo vilivyodumu kwa miezi tisa.

Chanzo kutoka ndani ya timu ya mazungumzo ya Israel, kilizungumza kwa sharti la kutotajwa jina, kilisema sasa kuna nafasi ya kweli ya kufikia makubaliano.

Jana,ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanjau, ilisema mazungumzo yataendelea wiki ijayo na kusisitiza kuwa tofauti bado zimesalia kati ya pande hizo.

Mzozo huo umesababisha vifo zaidi ya Wapalestina 38,000, kulingana na Wizara ya Afya ya Gaza.

**RFI**

## Starmer aanza kazi rasmi uwaziri mkuu Uingereza

**LONDON,** UINGEREZA

WAZIRI mkuu mpya wa Uingereza, Keir Starmer, ameanza majukumu yake mpya hii jana, baada ya kupata ushindi wa kishindo wa chama chake cha Labour katika uchaguzi mkuu uliofanyika Alhamisi.

Starmer alitumia saa zake za kwanza kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuunda baraza lake la mawaziri.

Pia jana aliongoza mkutano wake wa kwanza wa baraza la mawaziri na kuhudhuriwa na waziri wa fedha wa kwanza mwanamke, Rachel Reeves, na waziri mpya wa mambo ya kigeni, David Lammy.

Baada ya kuthibitishwa nafasi hiyo na Mfalme Charles 111, alitangaza kuanza kazi mara moja.

Chama cha Labour kilipata ushindi wa viti 412 vya bunge, ikiwa ni chini kidogo ya viti 418 ilivyovipata kwenye uchaguzi wa 1997 chini ya Tony Blair.

SAFU

MAKALA

# KERO HII YA MAWASILIANO KATIKA TAASISI IPATIWE MWAROBAINI



Na Magabilo Masambu

Mfano, umetuma cheti RITA kihakikiwe, tunatakiwa kujua kama kimepokewa, pili kila hatua mteja aone ili kuondoa wasiwasi kuhusu kushughulikiwa kwa tatizo lake.

UTAKUBALIANA na mimi kwamba dunia imepiga hatua kubwa katika mawasiliano. Kwa wale tuliyozaliwa kabla ya ujio wa mitandao ya kijamii na simu za mikononi, tutakuwa mashahidi namna tulivyopata tabu kuwasiliana miongoni mwetu.

Ninakumbuka baba yangu alikuwa akiniandikia barua kutoka Morogoro kuja Bunda, mkoani Mara. Ilichukua hata miezi mitatu kuipata, wakati mwingine ipotee kabisa, lakini leo mambo ni tofauti.

Kilichonifanya niandike makala hii si mawasiliano nyenyewe, bali namna ambavyo hatujaendana na dunia ya teknolojia hasa katika taasisi binafsi na za umma katika eneo la kupashana habari.

Mambo kadhaa yanaweza kuwa yanatokea hapa; uzembe, ushamba, majivuno.

Inawezekana kabisa, watu walioko kwenye baadhi ya vitengo hivyo vya mawasiliano ama hawana taaluma au wanataaluma lakini hawana uwezo wa kutoa huduma kwa mteja.

Ni jambo la ajabu na la ovyo sana, taasisi kufungua tovuti au kurasa kama vile Facebook, Instagram na kadhalika kisha kuweka ama email au namba za simu zisizopatikana au zinapatikana lakini hazipokewa.

Mtu mzima unajiuliza, hawa watu wanajitambua kweli? Kuanzia mkuu wa taasisi, kitengo cha mawasiliano na wote wanaohusika, kwamba mmeweka namba za simu zisizopatikana au zinapatikana lakini hampokei! Mnajua ni usumbufu gani mnasababisha kwa wateja wenu?

Kuweka mawasiliano maana yake ni kupunguza usumbufu wa watu walioko mbali na ofisi 'kuchoma nauli' zao ili kufika ofisini. Watu pia wanataka mrejesho, wakati mwingine huduma imecheleweshwa kwa makusudi au kutokana na mifumo ya kiteknolojia lakini inakuwaje simu zinapatikana na hazipokewi?

Kuna wakati unapiga simu ya taasisi ambayo imewekwa kwenye tovuti lakini mtu anapokea simu anasema mimi nilishahama hapo, nina miaka miwili siko pale. Unajiuliza hii ofisi ina watu kweli, hivi mtu anahama miaka miwili hambadilishi mawasiliano na ni ofisi inahudumia watu.

Malalamiko ya wananchi ni mengi dhidi ya baadhi ya taasisi kutotoa ushirikiano wa haraka katika kutatua changamoto hasa za kimawasiliano. Mfano, hivi sasa wanafunzi wengi wanaomba mikopo ya elimu ya juu, taasisi zote zinazohusika na suala hilo zimejipangaje kuhakikisha watu wanapata huduma kwa haraka au kupata mrejesho kwa haraka?

Mtu anatuma taarifa, hakuna mrejesho ndani ya wiki moja, mbili nakadhalika, akijaribu namba za simu zinaita bila kupokewa, tutafika kweli au tunarudi nyuma?

Kwa dunia ilivyo sasa, mtu hapaswi kuwa na wasiwasi kama taarifa zimefika au la. Kwanza, kwenye mifumo yote panatakiwa kuwekwa mifumo ya kujulisha wateja maendeleo ya utatuzi wa changamoto zao.

Mfano, umetuma cheti RITA kihakikiwe, tunatakiwa kujua kama kimepokewa, pili kila hatua mteja aone ili kuondoa wasiwasi kuhusu kushughulikiwa kwa tatizo lake.

Pengine tatizo ni watu kukosa taaluma ya huduma kwa wateja, nadhani kuna umuhimu wa wale wote waliosoma na wanaofanya kazi kwenye vitengo vya mawasiliano, kuhudhuria pia kozi za huduma kwa wateja, huko wafundishwe umuhimu wa kutoa huduma bora kwa mteja.

Unapokuwa ofisini tambua kila unayewasiliana naye ndiye bosi wako, siyo huyo anayekusimamia, kwa sababu hata anayekusimamia yupo hapo kwa ajili ya mteja, unampigia magoti bosi huyo wa ofisini na kumdharau mteja ambaye ndiye anayewafanya mlipwe mishahara.

Ushauri wangu kwa taaisi zote. Kama mnaamua kuweka mawasiliano kwenye tovuti zenu ni muhimu kufanya mawasiliano rafiki na wateja wenu, hao ndiyo wanaowafanya mnapendeza mkiwa ofisini.

Jambo la pili na kubwa, kama mmeweka namba za simu hakikisheni namba hizo zinapatikana na mnapokea vinginevyo hamfai kuwa ofisini. Ninyi ni mzigo tu kwa taasisi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam.**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kasheba alitabiriwa kifo, hakufa, akafariki alipojitabiria mwenyewe*



Na Adam Fungamwango

Mtu huyu ana mambo mengi ya kufurahisha, kupendeza, kushangaza na kusikitisha sana na historia yake, lakini tunachoangalia ni nyimbo mbili alizozitunga baada ya kuzushiwa kifo mara mbili kwa miaka ya tofauti.

HATA nikifa sitomaliza vifo wala sitojaza ardhi, nitakwenda kwenye kaburi langu mwenyewe, usiwe na wasiwasi na wewe lako lipo, kwa sababu na wewe ni marehemu mtarajiwa, linakusubiri.

Amekufa Masiya, wamekufa Mitume na Masultani, watawala wenye sifa, nguvu na pesa nyingi, sembuse mimi na wewe viumbe dhaifu, jamani tuhurumiane."

Ni maneno mazito yaliyotoka kinywani mwa mwanamuziki maarufu nchini tangu miaka ya 1970 alipofika nchini kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo hadi alipofariki mwaka 2004, Freddie Ndala Kasheba.

Mwanamuziki huyo aliyejizolea umaarufu mkubwa si kwa utunzi tu na kupiga gitaa la solo, bali pia ndiye mwasisi na kupiga gitaa la nyuzi 12, ambalo mashabiki wake walipachika jina la dazani, wengine wakaenda mbali zaidi wakalibatiza jina la kombora.

Kasheba aliyezaliwa 1946 na kufariki Oktoba 22, 2004 jijini Dar es Salaam, akiwa na miaka 18 sasa chini ya tumbo la ardhi ana historia ndefu kwenye muziki wa Tanzania na amekuwa na mchango mkubwa kwani huwezi kuuzungumzia muziki wa nchi hii bila kutaja mtu huyu aliyejizoelea sifa na mashabiki lukuki.

Mtu huyu ana mambo mengi ya kufurahisha, kupendeza, kushangaza na kusikitisha sana na historia yake, lakini tunachoangalia ni nyimbo mbili alizozitunga baada ya kuzushiwa kifo mara mbili kwa miaka ya tofauti.

Mwaka 1984 aliumwa na kulazwa kwenye Hospitali ya Agha Khan Dar es Salaam. Taarifa ambazo si za kweli zikasambaa kwamba amefariki dunia. Na hata baadhi ya bendi zilitangaza kifo chake kwenye kumbi ambazo zilikuwa zinapiga.

Siku mbili baadaye ilitokea picha yake kwenye gazeti la Mfanyakazi akiwa ameketi kwenye kitanda cha hospitali, juu kukiwa na maandishi, 'Sijafa'.

Alipona na alipotoka akatunga kibao kiitwacho 'Dunia Msongamano' ambacho kina mashairi kama yafuatavyo.

"Mawazo yamejia leo yaliyokuwa mzee wangu akisema, dunia ni msongamano wa watu wenye akili tofauti, ukitaka kuishi vema fikiri kabla ya kujibu, jifunze kwa waliwengu, waliwengu wajifuze kwako, dunia ni kuona mambo, halafu kuyasahau.

Mateso nimeshayapata, matatizo mengi yamenikuta, furaha nyingi nimeshaona, maisha nusu nimeshafanya, naelekea uzeeni sasa lazima niwe na utulivu, sababu kuishi kwingi, ni kuona mengi, kuelimisha watakaobaki ili waishi kwa heshima.

Dunia msongamani kasema baba , nimeyaona leo nakubali mimi. Wengine hupendelea kufurahia, wanaposikia fulani kafa oo, kufa kwa binadamu hupangwa na Mungu namuomba mwenyezi anipe maisha."

Walimwengu hawakuishia hapo. Mwanzoni mwa mwaka 2000 alikwenda kwao nchini Congo DR kusalimia.

Lakini zikaja taarifa za kizushi kuwa yuko hoi kwa kuumwa Kinshasa, wengine wakasema amefariki dunia, Ni taarifa zilizosambaa na kutangazwa sana kwani zililetwa na watu wa kuaminika.

Aliporejea nchini na kukuta anaitwa marehemu, aliionekana kukasirika, akachukua gitaa lake kombora na kutunga wimbo wa 'Yellow Card.'

Wimbo huu ambao aliimba kwa hisia kali, unatajwa kuwa ndiyo ilikuwa kama alijitabiria kifo, kwani haikuchukua miezi mingi, akafariki dunia.

"Zamani niliimba leo naimba dunia maajabu, Zamani niliimba leo naimba dunia matatizo, miaka ya 1980, walitangaza nimekufa, mwaka 2000 wakatangaza niko mahututi Kinshasa.

Nimeshazoa, imekuwa ni kawaida kila kukicha, wanamaarufu wana matatizo. Magonjwa yote ya dunia nimepachikwa mimi, wafurahi wao wenye uhakika wa afya njema, wataishi milele

Wakishakutana kwenye makontena kwenye vistoo kwenye kiti moto, ajenda maisha ya watu. Wakishakutana chini ya mwarobaini kwenye supu ya utumbo, mazungumzo yote utumbo. Fulani amekwisha, si lolote si chochote gari hana, mke kamkimbia kaenda zake Ulaya. Yote nakubali namuachia Mungu aliyeniumba, anajua mwisho wa maisha yangu. Kama dhidi yao nimecheza rafu, Mungu ndiye mwamuzi atanipa kadi 'Yellow Card', itakuwa ni onyo, kama ni nyekundu niondoke duniani, yote ni ya Mungu.

Jua linawaka mjini, nimepiga tai na shati jeupe natembea taratibu naogopa jasho wao wanasema siku hizi siwezi kutembea nimechoka. Eti jamaa yuko hoi hamalizi mwaka anaondoka huyo, tumpeleke tumpeleke.

Mwezao anaumwa wao wanacheka eti alikuwa na mali wache akome, kuzika wanashindana kuchanga tiketi ya ndege ipatikane haraka wakazike kijijini kwa sababu wakizika mjini wataota jinamizi.

Hata nikifa sitomaliza vifo wala sitojaza ardhi, nitakwenda kwenye kaburi langu mwenyewe, usiwe na wasiwasi na wewe lako lipo, kwa sababu na wewe ni marehemu mtarajiwa, linakusubiri.

Amekufa Masiya, wamekufa Mitume na masultani, watawala wenye sifa, nguvu na pesa nyingi, sembuse mimi na wewe viumbe dhaifu, jamani tuhurumiane."

Alifariki Oktoba 22, 2004 na kuzikwa kwenye makaburi ya Kinondoni, Dar es Salaam.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-1

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MWANANGU Shani, shule umemaliza, kidato cha nne. Kwa bahati mbaya hukubahatika kuendelea na masomo ya juu. Wazazi wako hatuna hata uwezo wa kukupeleka chuo chochote kile. Baba yako apeche alolo. Sasa sijui wewe moyoni mwako unawaza nini?"

"Kiukweli mama hata mimi mwenyewe hapa sielewi. Nilitamani nipelekwe chuo. Lakini niking'ang'ania nitawapa presha wazazi wangu. Najua uwezo wenu. Najua uwezo wa baba. Hawezi."

Mjadala huo wa Shani na mama yake Hanifa, ulifanyika nje ya nyumba yao, mmoja akiwa anachambua mboga za majani na mwingine akichambua mchele.

Mama alikuwa anachambua mboga za majani ili kuongezea maharage waliyobakiza mchana kwa ajili ya chakula cha usiku.

Shani alikuwa anachambua mchele kwa ajili ya kuanda chakula usiku. Wote walikuwa wamekaa kwenye mkeka.

"Usiniache nikalia mwanagu. Hata sisi wazazi wako tulipenda hivyo. Ukimsikia baba yako anavyolalamika utamuonea huruma. Lakini ataanzaje kwanza. Alitamani auze hata shamba lake moja kati ya mawili tuliyonayo. Lakini tutaishije? Shamba moja ni la mazao ya biashara yanayotupatia fedha za kujikimu, nguo na mahitaji mengine, moja ni la mazao ya chakula."

"Najua mama, ila mimi binafsi nilihitaji kusoma, lakini ndiyo hivyo tena!" Mama akamtazama binti yake aliyemaliza kuongea maneno hayo, halafu akamuuliza.

"Hivi, ukipata mchumba uko tayari kuolewa?" Akauliza kwa tahadhari.

"Ndiyo mama." Akaitikia kirahisi kuliko alivyodhani mama. "Lakini ni kwa yule ambaye nitampenda." Akaongeza kabla mama hajaongeza neno lolote.

Mazungumzo hayo ya mama na binti yake yalikuwa kwenye kijiji kimoja kiitwacho Lalanguru, kilichopo maeneo ya Ugalla, Kaliua mpakani mwa mikoa ya Tabora na Katavi.

Walikuwa nje ya nyumba iliyojengwa kwa udongo, lakini kwa ustadi mkubwa, ikinakshiwa na fito zilizokuwa zikizunguka nyumba hiyo mithili ya mistari ya pundamilia.

Kazi ya fito hizo, ilikuwa ni kuifanya nyumba kuwa imara, kwani ilifungwa kwa kamba za katani na nguzo za miti iliyoshikilia uimara wa nyumba yenyewe.




**"Hapa hapa kijijini!" Akajibu huku akitabasamu. Lilikuwa jibu moja. Mama akasubiri jibu la pili. Shukuru hakutaka kusema aliangua kicheko. "Niambie basi baba." Akabembeleza.**

Nyumba hiyo iliezekwa kwa bati ambazo hazikuwa na hata miezi sita, kiasi cha kuifanya kuonekana kung'aa kwa weupe mchana, nyakati za jua kali iwapo mtu ataiona akiwa mbali.

Wakati mwingine ilionekana kama iliyodondokewa na theluji. Wageni hawakupata tabu walipoelekezwa kwenye nyumba hiyo, au anayekwenda jirani ya maeneo hayo. Wakiambiwa kwenye nyumba yenye bati jeupe tu, basi ni hapo hapo kwa mzee Chilambo.

Katika kijiji hicho ni nyumba pekee iliyokuwa na bati jipya jeupe, kwani nyingi zilikuwa na mabati chakavu, yaliyogeuka rangi na kuwa ya kahawia kutokana na kuelezwa miaka mingi iliyopita bila kubadilishwa.

Uchakavu na kutu ndiyo iliyobadilisha mabati hayo kutoka weupe kwa kuwa rangi hiyo. Baadhi ya nyumba bado zilikuwa zimeezekwa kwa nyasi. Wenyewe walikuwa bado hawajapata uwezo wa kuezeka bati.

"Unasema?" Mama akauliza tena. "Nitakubali kuolewa mama, lakini ni kwa mwanamume ambaye nitaridhika naye."

"Mmmh!" Akaitikia mama na kuongeza "Wazo lako zuri mwanangu."

"Kwani yeye baba anasemaje?" "Mzee Chilambo ana neno basi! Niliongea naye kuhusu hilo, yeye sana sana anataka upate mchumba awe na uwezo wa kukutunza, mwenye uwezo, mwenye mali, ambaye anaweza hata kutusaidia sisi wazazi." Shani akashtuka. Akamwangalia mama yake kwa mshangao. "Mwenye mali!?" Akauliza kwa mshangao. "Ndiyo! Mwenye pesa, hataki binti yake achukuliwe na mtu aende akapate tabu huko, binti yake akadhalilika. Sijui uko tayari binti yangu?" Mama akamuuliza. Akashusha pumzi nzito na kuitikia kama kalazimishwa, "haya."

Uitikiaje ule ulimfanya Bi. Hanifa kuona kama kuna kitu ambacho binti yake hakuridhika nacho. Lakini hakutaka kumwambia chochote. Badala yake akahamisha mada.

************************************

"Mama mimi nina jambo nataka nikwambie." "Nini tena mwanangu mbona unanitisha?"

Wakakaa chini. "Mama mimi nataka kuoa!" "Kuoa?" Akashangaa huku akimwangalia kijana wake usoni. "Ndiyo mama, nimeshafika umri wa kuoa mimi."

"Najua mwanangu umeshakuwa mkubwa, lakini ndoa siyo kitu cha masihara. Siyo cha kukichukulia mzaha, inabidi uwe umejipanga kweli kweli."

"Mama kwani unaona siwezi kukaa na mke?" "Mhh, naona kama akili yako haijakomaa mwanangu, unakwenda kuishi na mwanamke ambaye hujazaliwa naye, ametoka kwenye malezi tofauti?" "Naweza mama, unaniona hivi." "Mhh mwanangu, unataka kujibebea majukumu bado mdogo hivyo, haya sikukatazi."

Mazungumzo hayo ya kijana Shukuru na mama yake Bi. Rehema yalifanyika ndani ya kijiji hicho hicho cha Lalanguru.

Walikuwa nje ya nyumba chakavu. Ilikuwa ya udongo, lakini baadhi ya maeneo ulikuwa umenyofoka na kufanya matobo matobo mengi. Sehemu zenye matobo zilizibwa kwa kutumia mifuko tupu ya saruji na viroba.

Nyumba hiyo ilionekana ilijengwa siku nyingi sana na wenyewe hawakuwa wakiifanyia ukarabati hata wa kuchukua udongo na kukandika maeneo yenye matobo. Kama si vifuko na viroba basi watu wangeweza kuona kilichomo ndani. Ilikuwa imeezekwa nyasi ambazo nazo tayari ziliiliwakuwa zimeshabadilika rangi na kuwa nyeusi.

"Enhee nani tena unataka kumuoa? Wa hapa hapa kijijini au?" Bi. Rehema akauliza maswali mawili kwa wakati mmoja.

"Hapa hapa kijijini!" Akajibu huku akitabasamu. Lilikuwa jibu moja. Mama akasubiri jibu la pili. Shukuru hakutaka kusema aliangua kicheko. "Niambie basi baba." Akabembeleza.

"Shani!" Akajibu kwa sauti ya upole. Mama akamuangalia kwa makini usoni mwanaye. Halafu akamwabia "Mhh, mwanangu nikasichana kazuri sana kale. Kwani vipi si kamemaliza shule kidato cha nne, hakaendelei?" "Hapana, wazazi wake wameshindwa kumuendeleza, kasema yeye yupo nyumbani tu." "Sawa, lakini baba yake wewe unamuoneje?" "Kwani yukoje mama?" "Mzee mkorofi na mtata yule, sijui kama mtawezana. Vizuri lakini mwanangu umechagua msichana mzuri, ana heshima na adabu. Mimi kama mama yako nitajitahidi kusukuma kupiga ndogo ndogo kwa mama yake ili barua tutakayoipeleka ikubaliwe."

"Ndiyo ninachokupendea hicho mama." Shukuru akasema huku akimkumbatia mama yake.

"Baba je sasa?" "Huyo niachie mimi. Ila kwa hili sidhani kama atapinga."

"Sawa mama hilo ndilo nililokuitia huku pembeni tutete, fanya kweli basi mama nakuamini, mimi natoka kidogo, nikirudi lazima nikuletee samaki kwa furaha yangu kesho tupike na ubwabwa."

"Haya mwanangu, umekuwa sasa baba." Bi. Rehema aliamuangalia kijana wake wakati anaondoka nyumbani hapo.

Alipofika hatua kadhaa mbele, aligeuka nyuma na kukuta bado mama yake amesimama pale pale anamtazama. Akamuonyesha ishara kwa dole gumba, kuwa anamkubali na kumpenda sana mama yake.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# OTILE AGEUKIA WANAOJUA KISWAHILI

MKALI wa muziki wa kizazi kipya kutoka Kenya, Otile Brown, ametoa nafasi ya kumsaidia msanii yeyote chipukizi kutoka nchini humo mwenye uwezo wa kuimba kwa lugha ya Kiswahili.

Kulingana na ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo aliyejijengea sifa nchini humo amesema ameamua kumsaidia msichana mwenye sifa hizo kufikisha kipaji chake katika daraja la juu kisanaa.

"Natafuta msanii wa kike kutoka sehemu yoyote ya Kenya ili mradi tu unajua kuimba Kiswahili kizuri. Rafudhi ni muhimu kwenye nyimbo zetu za kiswahili," aliandika Otile.





# DIAMOND AONYESHA UKUBWA WAKE

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amezidi kuonyesha kwamba yeye sio mtu wa kawaida, baada ya kuonekana akiwa karibu na staa wa soka wa Ufaransa, Poul Pogba.

Mastaa hao wawili ambao wako Dubai, walionekana hivi karibuni wakifurahi pamoja kwa kuangalia mechi hiyo ya robo fainali ya Euro 2024.

Katika mechi hiyo Ufaransa waliwachapa Ureno katika mikwaju ya penalti na kufuzu kwa hatua ya nusu fainali.

"Wakati wa sherehe kwa Ufaransa @paulpogba @diamondplatnumz," aliandika Diamond chini ya video hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### EDERSON ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kupokea ombi kutoka Saudi Arabia kumnunua mlinda mlango Ederson na wanataka zaidi ya pauni milioni 30 kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye anahusishwa na klabu ya Al-Nassr. (**Sportsport**)

### MASON AWANIWA MARSEILLE

MARSEILLE ina uhakika wa kuwashinda Lazio kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood baada ya klabu hiyo ya Serie A kutoa pauni milioni 17 kwa mchezaji huyo wa miaka 22. (**Mail**)

### PAQUETA AWEKWA OKONI

KLABU ya Famengo imeanza mawasiliano na West Ham kuhusu usajili wa mchezaji wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, Lucas Paqueta, klabu hizo mbili ziko katika hatua za awali za mazungumzo hayo. (**Globo**)

### WILLIAMS ANUKIA BARCA

BARCELONA inaongoza mbio za kumsajili winga wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams, huku Arsenal na Chelsea wakikabiliwa na hatari ya kumkosa mchezaji huyo. (**Football Insider**)

### CUCURELLA AMSHAWISHI WILLIAMS

MLINZI wa Chelsea, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 25, amesema anajaribu kumshawishi mchezaji mwenzake wa Hispania, Nico Williams ajiunge na The Blues, wawili hao wapo kwenye kikosi cha nchi yao kwenye Euro 2024. (**Sport**)

### YORO AITAKA REAL MADRID

MLINZI wa Lille, Leny Yoro anataka kuhamia Real Madrid na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 18 anasubiri klabu kuafikiana, wakati Liverpool na Paris St-Germain ziko tayari kumnyakua iwapo dili hilo litasambaratika. (**Fabrizio Romano**)

### MATTY AOTA MBAWA MILAN

MLINZI wa kulia wa Aston Villa, Matty Cash huenda asijiunge na AC Milan licha ya ripoti zinazomhusisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 26 na klabu hiyo ya Serie A. (**Birmingham Live**)

### BARCA YAMTAKA JOAO CANCELO

KLABU ya Barcelona ina nia ya kumsajili Joao Cancelo wa Manchester City baada ya beki huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 30 kucheza kwa mkopo katika klabu hiyo ya Hispania msimu uliopita. (**SportsMole**)

### KOOPMEINERS ATAKIWA JUVE

JUVENTUS inataka kuimarisha safu yao ya kati kwa kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 26, Teun Koopmeiners. (**La Gazzetta dello Sport**)

### LUSALE AWINDWA MAN UTD

KLABU ya Manchester United inakaribia kumsajili kinda mwenye umri wa miaka 16 kutoka Slovakia, Samuel Lusale kutoka Crystal Palace. (**Moror**)

### DOMINIC BASI TENA

USAJILI wa Newcastle United wa mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, umegonga mwamba baada ya Magpies kushindwa kumuuza mshambuliaji wao, Callum Wilson. (**Telegraph**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CANADA YAIFUATA ARGENTINA NUSU FAINALI COPA AMERICA

**NEW JERSEY,** Marekani

**● ● ● Ni baada ya kupambana vikali kwenye mechi ya robo fainali dhidi ya....**

CANADA ilishinda kwa penalti 4-3 dhidi ya Venezuela juzi Ijumaa na kutinga nusu fainali ya Copa América katika mechi yao ya kwanza baada ya mchuano mkali ulioishia kwa sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 120.

Huku timu zikiwa zimesawazisha baada ya majaribio matano kila mmoja, Wilker Ángel alifunga mkwaju wake wa penalti uliookolewa na Maxime Crepeau kwenye mikwaju ya penalti na Ismael Kone akafunga penalti ya ushindi na kuipeleka Canada nusu Fainali.

"Hisia zinazidi kupanda, nina furaha sana kwa kila mtu ambaye anatuunga mkono," alisema Crepeau, ambaye aliokoa mara mbili kwenye mikwaju hiyo, akimwambia mtangazaji wa Canada TSN.

"Ni kazi kubwa na sasa tuna matunda ya bidii yetu. Hii inashangaza kuwa katika nusu fainali ya Copa América. Nadhani kila mtu anahitaji kutambua nchi hii na wanasoka wake wanastahili heshima."

Canada itamenyana na Argentina mjini New Jersey siku ya Jumanne kuwania nafasi ya kucheza fainali ya Julai 14.

Nusu fainali hiyo itakuwa ni mechi ya marudiano ya ufunguzi wa michuano hiyo, ambapo mabingwa watetezi Argentina waliibuka na ushindi wa mabao 2-0.

**Timu hiyo ya Amerika Kaskazini imekuwa timu ya nne ya Concacaf kufika nusu fainali ya Copa América, baada ya Mexico, Honduras na Marekani.**

Canada, ambao walifunga bao moja pekee katika mechi zao tatu za hatua ya makundi, walianza mechi hiyo kwa kasi na kupata katika dakika ya 13 lililofungwa Jacob Shaffelburg alipounganisha krosi ya Jonathan David.

Baada ya kufunga bao, Shaffelburg aliishika jezi ya mchezaji mwenzake Tajon Buchanan, ambaye alivunjika mguu mazoezini wiki hii.

Vijana wa kocha, Jesse Marsch walipoteza nafasi kadhaa za kuendeleza uongozi wao katika kipindi cha kwanza, huku Shaffelburg wakimjaribu kipa Rafael Romo kutoka pembeni mwa eneo huku David akituma juhudi nje ya lango baada ya kujipata kupitia moja kwa moja.

Venezuela walijikakamua kutafuta goli na walikuwa na uwezo wa kumiliki mpira zaidi, lakini walipunguza kwa kiasi kikubwa krosi za kubahatisha na mashuti ya mbali, huku mfungaji bora wa muda wote, Salomón Rondón akichomoa mara mbili kuokoa kutoka kwa Crepeau.

Hatimaye Venezuela walipata bao la kusawazisha katika dakika ya 64 kupitia kwa Rondon.

Lilikuwa bao la 44 la mshambuliaji huyo wa zamani wa Everton na Newcastle United kwa Venezuela.

Canada walijibu vyema bao la kusawazisha na mchezaji wa akiba Liam Millar aliokoa mpira dakika ya 67 kabla ya Tani Oluwaseyi kupiga mashuti mawili juu ya lango katika muda wa dakika nne, lakini hakuna timu iliyoweza kupata ushindi katika muda wa kawaida.

# MARTINEZ: RONALDO BADO HAJAAMUA MUSTAKABALI WAKE URENO



**HAMBURG,** Italia

KOCHA wa Ureno Roberto Martínez amesema "ni mapema sana" kusema Cristiano Ronaldo alikuwa ameichezea nchi yake mechi yake ya mwisho kufuatia timu hiyo kutolewa kwenye michuano ya Euro 2024 na Ufaransa mjini Hamburg juzi Ijumaa.

Ureno ilishindwa kwa mikwaju ya penalti 5-3 katika robo fainali baada ya suluhu kwenye dakika za kawaida ambapo Ronaldo alikosa nafasi katika muda wa ziada lakini akafunga moja ya mikwaju hiyo.

"Ni mapema sana baada ya mechi kuzungumzia hilo na hakujakuwa na maamuzi ya mtu binafsi," alisema Martínez kwenye mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa ikiwa ulikuwa ni mchezo wa mwisho wa Ronaldo akiwa na jezi ya Ureno.

Pale kwenye uwanja wa Volksparkstadion ilikuwa mechi ya 212 kwa Ronaldo.

Mabao yake 130 kwa nchi yake ndiyo mengi zaidi katika soka la kimataifa huku Lionel Messi hivi majuzi akishika nafasi ya pili kwenye orodha hiyo akiwa na mabao 108.

Hata hivyo, Ronaldo mwenye umri wa miaka 39 alitatizika kufufua magwiji wa zamani katika michuano hiyo nchini Ujerumani na kuondoka Euro 2024 bila kufunga bao tofauti na penalti.

Ilikuwa ni mara ya kwanza katika maisha yake ya soka kwa Ronaldo kushindwa kufunga katika michuano mikubwa ya kimataifa, na mashuti yake 10 bila kufunga.

Maisha ya Ronaldo ya miaka 20 kwenye michuano ya Euro yalijumuisha taji la 2016 -- wakati Ureno ilipoishinda Ufaransa katika fainali -- na bado haijafahamika iwapo mchezaji huyo bora wa dunia mara tano ataendelea kuichezea nchi yake hadi 2026 kwenye Kombe la Dunia, wakati ambapo atakuwa na umri wa miaka 41.

Alisema kufuatia ushindi wa Ureno wa hatua ya 16 bora dhidi ya Slovenia kwamba kuvunja rekodi yake ya kucheza mara sita michuano ya Ulaya itakuwa mwisho wake.

"Bila shaka ni Euro ya mwisho kwangu, bila shaka ndiyo," alisema Ronaldo akiiambia RTP ya Ureno.

"Lakini halina hisia. Nimeguswa na kila kitu kinachohusu soka, kwa shauku niliyonayo kwa mchezo, shauku ninayoiona kwa mashabiki, kuwa na familia yangu hapa, mapenzi ya watu ... Nikiacha ulimwengu wa soka. Ni nini kingine ninachoweza kufanya au kushinda?"

## Murray aaga rasmi mchezo wa Tennis

**LONDON,** England

BINGWA wa zamani wa Wimbledon, Andy Murray amewashukuru waandaaji wa mashindano hayo kwa hafla iliyojawa "kihisia kali" ya kumuaga baada ya kucheza kwa mara ya mwisho katika mashindano hayo yenye hadhi na heshima ya juu ya tenisi duniani.

Bingwa huyo mara mbili mashindano hayo anacheza katika Klabu ya All England kwa mara ya mwisho kabla ya kustaafu baadaye mwaka huu.

Video yake ya zamani ya uchezaji ilichezwa kwenye 'skrini' kubwa iliyokuwa eneo la uwanja mkuu yaani Centre Court baada ya mechi kumalizika, jambo lililomfanya mchezaji huyo bora wa zamani wa dunia kulia huku maelfu ya mashabiki wakionesha shukrani zao kwa kupiga makofi mengi.




"Naona kama mwisho mzuri kwangu. Ikiwa ninastahili tukio hili au la, sijui. Lakini waandaaji walifanya kazi nzuri sana," alisema Murray, ambaye alishinda Wimbledon mwaka wa 2013 na 2016 huku familia yake ikifika kwenye uwanja huo mkuu uliojaa watu.

Murray aliishukuru familia yake, washiriki wa timu yake kwa miaka mingi na mashabiki kwa uungwaji mkono usiokoma.

"Ni ngumu kwa sababu nataka kuendelea kucheza, lakini siwezi, Kimwili ni ngumu sana. Nataka kucheza milele. Naupenda huu mchezo," Murray alisema.

# Hispania ina njaa na Euro 2024 - Kocha



**STUTTGART,** Ujerumani

KOCHA wa Hispania, Luis de la Fuente amesema wachezaji wake "hawajatosheka" na wanataka mafanikio zaidi kwenye Euro 2024 baada ya kuweka historia kwa kuwaondoa wenyeji Ujerumani kwenye Uwanja wa Stuttgart Arena Ijumaa.

Mikel Merino alifunga bao la ushindi dakika ya 119 wakati Hispania ilipowalaza wenyeji katika mchuano mkubwa kwa mara ya kwanza katika majaribio 10 baada ya Florian Wirtz kusawazisha bao la kwanza la Dani Olmo katika muda wa kawaida.

Hispania itakutana na Ufaransa katika nusu fainali mjini Munich Jumanne, na De la Fuente anatumaini kuwa mbio zao zitaendelea hadi fainali mjini Berlin mnamo Julai 14.

"Tunaona historia," alisema kocha huyo katika mkutano na wanahabari baada ya mchezo huo. "Ni mara ya kwanza tumepata ushindi mara tano mfululizo kwenye Euro.

"Pia ni mara ya kwanza kuwashinda wenyeji katika moja ya mashindano makubwa. Ni wakati wa kuweka thamani kwa kile tulichofanikiwa na kufurahia wakati huu wa kihistoria.

"Tutaona jinsi stori itaisha, lakini timu hii inataka kufika mbali zaidi, wachezaji hawa wana moyo, hawatosheki, hawachoki kushindana na kufanya kazi kwa bidii, wana tamaa, ni heshima kuwa na wachezaji kama hawa."

Hispania hapo awali walitatizika dhidi ya wenyeji kwenye michuano mikubwa, kwani walipoteza katika Fainali za Kombe la Dunia na Urusi mnamo 2018 na Korea Kusini mnamo 2002, huku pia walifungwa kwa uchungu na Ufaransa kwenye fainali ya Euro 1984.

Huzuni zaidi ilionekana kufuatwa huko Stuttgart Wirtz alipoisawazishia Ujerumani na kupeleka mchezo katika muda wa ziada baada ya Olmo kugeuza krosi ya Lamine Yamal.

Bao la dakika za lala salama la Merino liliifanya Hispania kuwa juu ya mstari mwishoni, lakini De la Fuente bado alihojiwa ni kwa nini aliwatoa Yamal na Nico Williams, miongoni mwa wengine, baada ya kuongoza, kuondoa tishio la La Roja kwenye kaunta.

"Inategemea ikiwa ni vizuri kukimbia au la," alijibu. "Tumeonesha kwamba bila kukimbia sana, tulishinda mchezo. Tulihitaji kukimbia kidogo."

HABARI MICHEZO

# MTASINGWA ARIPOTI AZAM FC

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya tetesi kutaka kujiunga na mabingwa wa soka nchini, Yanga, kiungo Adolf Mtasingwa ameripoti kwenye kikosi cha timu yake ya Azam kilichoanza mazoezi kujiandaa na msimu mpya.

Hivi karibuni, Mtasingwa alikuwa akihusishwa kutaka kujiunga na Yanga baada ya mabingwa hao kuvutiwa na uwezo wake aliouonyesha kwenye kikosi cha Azam na timu ya taifa 'Taifa Stars'.

Hata hivyo, dili hilo ni kama limekufa baada ya kiungo huyo juzi Ijumaa kuripo kwenye mazoezi ya timu yake ya Azam FC kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na Nipashe, Afisa habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka', alisema kuwa nyota huyo ni miongoni mwa wachezaji wao walioripoti mazoezini.

"Tumeanza mazoezi kujiandaa na msimu mpya na mashindano ya kimataifa, wachezaji wote wa Azam FC wameripoti, kama nilivyosema kwa sasa tetesi zitakuwa nyingi, lakini kama Azam tunaendelea na maandalizi yetu," alisema Zaka.

Aidha, alisema baada ya mazoezi ya siku kadhaa Dar es Salaam, kikosi hicho kitaelekea Zanzibar na baadae Morocco kujiwinda na Ligi Kuu na michuano ya Kimataifa.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunafanya vizuri msimu ujao kwenye mashindano yote tutakayoshiriki, tunaamini maandalizi mazuri yanakupa matokeomazuri baadae," alisema Zaka.

Azam msimu ujao itashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Yanga baada ya kumaliza Ligi kwenye nafasi ya pili nyuma ya mabingwa hao.

Klabu za Simba na Coastal Union zenyewe zitaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombela Shirikisho Afrika baada ya kumaliza Ligi kwenye nafasi ya tatu na ya nne.



Kiungo wa Azam FC, Adolf Mtasingwa (kushoto) akiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo juzi kujiandaa na msimu mpya. **PICHA:BINZUBEIRY**

# Mbangula atamani kuitwa Stars

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI wa klabu ya Prisons, Samson Mbangula, amesema anatamani sana kuitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa 'Taifa Stars'.

Mbangula amebainisha kuwa tangu aanze kuichezea Prisons katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu sita, hajawahi kuitwa kwenye kikosi hicho, hivyo anaona kama ni wakati wake sasa wa kwenda kutoa mchango wake katika timu hiyo.

Amewataka wasimamizi na jopo la makocha wa Stars kuangalia zaidi wachezaji ambao wako kwenye kiwango cha juu kwa wakati husika ili nao wawe na mchango kwenye kikosi cha nchi yao.

Mbangula amesema hayo siku chache tu baada ya droo ya makundi kusaka tiketi ya kucheza michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025 itakayofanyika nchini Morocco huku Taifa Stars kupangwa kundi H, ikiwa pamoja na timu za Ethiopia, Guinea na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

"Mimi nafikiri wale wasimamizi na jopo la makocha wa Taifa Stars wawe wanaangalia wachezaji walio kwenye viwango vya juu kwa muda huo, kwa sababu sisi wachezaji wakati mwingine unakuwa juu, au unashuka kiwango kwa sababu ya majeraha, sasa unapokuwa kwenye ubora unatakiwa uisaidie Stars, mimi nipo tayari kwa wakati huu, haya yote nasema kwa sababu ya maslahi mapana ya taifa," alisema mshambuliaji huyo.

Alisema Ligi Kuu msimu uliomalizika alifanikiwa kufunga mabao manane, akishika nafasi ya pili kwa mabao mengi upande wa washambuliaji wazawa nyuma ya Waziri Junior aliyemaliza na mabao 12.

Rekodi zinaonyesha kuwa msimu wa 2019/20 alipachika mabao manane, akafunga matatu msimu wa 2020/21, bao moja msimu wa 2021/22 na mabao sita msimu wa 2022/23, kabla ya kufunga manane msimu uliopita.

## Wahimizwa kushiriki michezo

**Na Faustine Feliciane**

GOLIKIPA wa klabu ya Simba anayehusishwa kutaka kujiunga na Azam FC, Aishi Manula, amesema ni vizuri kwa watu kushiriki michezo ili kujenga afya.

Akizungumza jana kwenye maonyesho ya biashara ya sabasaba wakati akikabidhi zawadi kwa washindi Zigo la Euro 2024, Manula aliwataka watu kujihusisha na michezo pamoja na kuchangamkia fursa mbalimbali kwenye michezo.

"Ushiriki katika michezo una faida kubwa, watu wafanye mazoezi lakini pia wafuatilie michezo kwa sababu ndani kuna fursa nyingi, kama leo nakabidhi zawadi kwa washindi wa wa Zigo la Euro," alisema Manula.

Nyota huyo alipongeza kampuni ya Tigo kwa kuwaweka watu karibu na michezo kwa kuanzisha kampeni mbalimbali zinazowanufaisha wananchi mbalimbali.

"Sasa hivi kuna michuano ya Euro 2024 inafanyika Ujerumani, watu wanafuatili kwa karibu na kuna timu wanazozishangilia, kampeni kama hizi zinawafanya watu kuwa karibu na mashindano mbalimbali yanayoanzishwa.

Kwenye michuano hiyo ya Euro inayoendelea Ujerumani, baadhi ya mashabiki wamepata fursa ya kwenda kuangalia hatua ya robo fainali kupitia kampeni hiyo.

## Mashine za Yanga zatua nchini, yatamba kuwa tishio Afrika

INATOKA UK. 24

gazwa ni, Jean Baleke, anayekuja kuchukua nafasi ya Joseph Guede ambaye anaondoka kwa kile kilichoelezwa amemaliza mkataba na hakutaka kuongeza baada ya kupata timu Falme za Kiarabu.

Mpaka sasa Yanga imemtangaza rasmi mchezaji mmoja tu ambaye ni Chama, raia wa Zambia, lakini ikihusishwa na wachezaji wengine kadhaa.


Wachezaji hao ni Emmanuel Lobota, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anayechezea Singida Black Stars, na Wakongo wengine ambao ni Agee Basiala, kiungo mshambuliaji na Onoya Sangana Charve kiungo mkabaji wote kutoka AS Maniema Union pamoja beki wa kushoto, Chadrack Boka kutoka klabu ya Saint Eloi Lupopo.

Wengine ni Chikamso Okechukwu, beki wa kati kutoka Enyimba, Prince Dube na kipa, Khomein Aboubakar kutoka Singida Black Stars.

# Michezo

Jumapili Julai 7, 2024

Nipashe



UK. 22

**Martinez: Ronaldo bado hajaamua mustakabali wake Ureno**



Mshambuliaji wa timu ya taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe (kushoto) akiwania mpira na beki wa Ureno, Palhina kwenye mchezo wa robo fainali ya michuano ya 'Euro 2024' juzi usiku, Ureno walitolewa kwenye hatua hiyo kwa mikwaju ya penalti. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yafuata makali Misri, yashusha kiungo mkabaji

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

## Yamsainisha kiungo mkabaji kutoka Nigeria, kurudi nchini siku chache kabla ya....

KLABU ya Simba inatarajia kuondoka kesho kuelekea Misri kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na msimu mpya huku ikikamilisha usajili wa kiungo mkabaji Augustine Okajepha kutoka klabu ya Rivers United ya Nigeria.

**Uongozi wa klabu hiyo, umeamua kuipeleka timu hiyo Misri ili kufuata utulivu na kuwapa nafasi makocha wa timu hiyo kuingiza mbinu zao kwa wachezaji.**

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema uongozi unaamini kambi ya timu hiyo nchini Misri itakuwa yenye tija na kuandaa kikosi bora kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa.

"Tumepania kurudisha furaha kwa mashabiki na wanasimba wote, tunaenda kuweka kambi Misri katika mji wa Ismailia na makocha wetu watapata fursa ya kuandaa timu kwenye mazingira tulivu, msimu ujao utakuwa msimu wa Simba," alisema Ahmed na kuongeza,

"Kutakuwa na semina na kuwandaa kisaikolojia wachezaji, wataambiwa historia ya Simba na nchi ya Tanzania, ukubwa wa klabu, vitu ambavyo imeshawahi kuvifanya huko nyuma na malengo yake ya baadaye," alisema.

Alisema kambi hiyo itafanyika mpaka siku chache kabla ya tamasha la Simba day lililopangwa kufanyika Agosti 3 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kwenye kilele cha tamasha hilo la kila mwaka, Simba inatarajia kucheza mchezo maalum wa kirafiki dhidi ya APR ya Rwanda.

Kuhusu usajili, Ahmed alisema wanawendelea kushusha 'vifaa' baada ya kukamilisha usajili wa Okajepha.

"Ni rasmi tumekamilisha usajili wa kiungo mkabaji, Okajepha, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Rivers United ya Nigeria, tumempa miaka mitatu, nadhani sasa baada ya kuhangaika sana ndiyo tumempata mtu sahihi eneo la ukabaji, Simba itakuwa imara kwa sababu kwenye mpira wa kisasa kama huna kiungo mkabaji aliyekamilika, basi timu yako itahangaika sana, na ndiyo timu yetu ilivyokuwa misimu mitatu iliyopita," alisema.

Alibainisha kuwa kwa muda mrefu walikuwa wanasajili wachezaji ambao walishindwa kulitendea haki eneo hilo.

"Kwa muda mrefu Simba tumekuwa tukihangaika na wachezaji wa eneo hilo, kwa maana ya kiungo mkabaji, tulikuwa na Mganda Thadeo Lwanga alifanya vizuri sana, baadaye alipopata majeraha akashindwa kurejea kwenye ubora wake, akaja Mbrazil Gerson Fraga naye akawa majeruhi, awali kulikuwa na Mghana James Kotei, akafanya vizuri sana, mbele huko ubora ukapungua akaondoka, tukaleta wengine hapa katikati wakashindwa kukata kiu ya wanachama na mashabiki wa Simba, sasa tumetibu tatizo kwani ameonyesha kuwa ni mchezaji mzuri huko alikotoka," alisema Ahmed.

Kabla ya kujiunga na Rivers United, 2023, mchezaji huyo alikuwa akiichezea, Kano Pillars aliyojiunga nayo mwaka 2021 ambapo klabu hiyo ilimsajili kutoka Warri Wolvers, zote za nchini humo.

Kabla ya mchezaji huyo, Simba iliwatangaza wachezaji wapya, winga Mzambia Jushua Mulate, mshambuliaji Mganda, Steven Mukwala, na Jean Charles Ahoua raia wa Ivory Coast.

Kwa upande wa wazawa, tayari imeshawatangaza beki wa kati, Lameck Lawi, Abdulrazack Hamza na Valentino Mashaka.

Hata hivyo jana jioni Simba ilitarajiwa kutangaza usajili wa wachezaji wengine wawili ilitarajia kutangaza wachezaji wengine wapya wawili, jioni na usiku.

## Mashine za Yanga zatua nchini, yatamba kuwa tishio Afrika

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga wakiwemo wapya waliosajiliwa hivi karibuni kuelekea msimu ujao wa mashindano wameanza kuwasili nchini kwa ajili ya kuripoti kambini kesho Jumatatu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe amesema wachezaji wote walipewa taarifa ya kutakiwa kuwa nchini kufikia leo Jumapili ili kumpa nafasi Kocha Mkuu, Miguel Gamondi aanze kazi ya kukisuka kikosi kwa ajili ya michuano ya ndani na ile ya kimataifa.

"Wachezaji wameshaanza kuwasili nchini kuanzia leo (jana), wapo ambao tayari wametua, wengine kesho (leo), hii ni kwa wote wapya na wale tulioongezea mikataba, kocha alitaka wachezaji wote wawe wamewasili kambini Kigamboni Jumatatu (kesho), kwa ajili ya maandalizi ya msimu," alisema Kamwe.

Amewahakikisha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuwa hivi karibuni wanatarajiwa kutangaza mchezaji mwingine ambaye atatikisa nchi kama ilivyokuwa na Clatous Chama, huku akitamba kuwa kikosi kitakachoundwa kwa msimu ujao kitakuwa tishio Afrika, mara mbili zaidi ya kile cha msimu uliopita.

"Tumewabakisha wachezaji wetu bora, tumefanya hivyo kwa asilimia 90, bado asilimia 10 tu, baada ya hapo tunakwenda kupiga pigo la pili, hili ni zaidi ya lile la kwanza.

"Kuelekea msimu ujao tunataka kutengeneza timu ya kutisha, ya wachezaji ambao wanawaza kwenda kuchukua medali, kama nilivyotangulia kusema hapo nyuma kuwa lengo letu kuelekea msimu unaokuja ni kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, fainali, au kutwaa ubingwa kabisa," alisema.

Habari zinasema mchezaji anayetajwa kuwa anaweza kutan-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >